JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

# Muhtasari wa Somo la Kiswahili kwa Elimu ya Sekondari

## Kidato cha I - IV

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

## MUHTASARI WA SOMO LA KISWAHILI KWA ELIMU YA SEKONDARI

## KIDATO I - IV

2005

© Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, 2005
Chapa ya kwanza 2010
Chapa ya pili 2012
Chapa ya tatu 2016

**ISBN 978 - 9978 - 61 - 293 - 9**

Umebuniwa na kutayarishwa na:

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P 35094
Dar es Salaam
TANZANIA

Simu: +255 -022 - 2773005/2774420 /2780891
Nukushi: +255 -51-2774420
Barua pepe: director.tie@tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kukitoa kitabu hiki kwa jinsi yoyote ile bila idhini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya ufundi.

## YALIYOMO

**Ukurasa**

Utangulizi ........................................................................................ iv

Malengo ya Elimu Tanzania ........................................................................v

Madhumuni na Malengo ya Elimu ya Sekondari ........................................ vi

Umahiri wa jumla wa somo la Kiswahili........................................................vi

Malengo ya jumla ya kufundisha somo la Kiswahili Sekondari .................... vii

Muundo wa Muhtasari .................................................................................vii

Kidato cha Kwanza ........................................................................................ 1

Kidato cha Pili ............................................................................................ 28

Kidato cha Tatu ........................................................................................... 56

Kidato cha Nne ............................................................................................ 76

## 1.0 UTANGULIZI

Muhtasari huu wa Kiswahili kidato cha kwanza hadi cha nne utatumika badala ya ule wa mwaka 1997.

Muhtasari wa somo la Kiswahili kwa shule za sekondari uliopita ulitolewa mwaka 1997. Katika kipindi chote cha utekelezaji wa muhtasari huo, mabadiliko mengi yametokea katika nyanja mbalimbali zikiwemo za siasa, sayansi, teknolojia, uchumi, utamaduni na elimu. Mabadiliko yanapotokea huathiri lugha na ufundishaji wake.

Muhtasari huu umezingatia masuala ya kitaaluma, kijamii na kiteknolojia yanayojiri sasa. Masuala hayo ni pamoja na masuala mtambuko, mbinu shirikishi za kujifunzia na kufundishia na msamiati. Aidha muhtasari umezingatia muhamo wa ruwaza unaohusu mkabala wa ufundishaji na ujifunzaji unaomjali mwanafunzi na uliojikita katika ujuzi na utendaji wa mwanafunzi.

## 1.1 Ushauri kwa mwalimu:

Mada za muhtasari huu zimepangwa kuliangana na vidato. Inashauriwa kuwa mada hizi zifundishwe kwa njia ya kuzichanganya na si kwa kufuata mtiririko wa mada uliomo kwenye muhtasari. Kwa mfano, katika wiki moja, mwalimu anaweza kufundisha vipengele vya fasihi kwenye kipindi kimoja, sarufi katika kipindi kingine na utungaji katika kipindi kingine. Kwa hiyo ni vema mwalimu aandae azimio la kazi kwa utaratibu huo.

Pia mwalimu anashauriwa kuzingatia yafuatayo:-

a) Pamoja na njia/mbinu za kufundishia na kujifunzia zilizoandikwa humu, mwalimu abuni njia nyingine kulingana na uwezo na vionjo vya wanafunzi wake, kwa kuzingatia njia/mbinu shirikishi zinazowashughulisha wanafunzi.

b) Atengeneze na kutumia zana na vifaa vya kufundishia kulingana na mahitaji ya wanafunzi wake..

c) Ajielimishe kwa kusoma maandiko mbalimbali yanayochapishwa kila wakati.

d) Awe mfano mzuri wa kuzungumza na kuandika Kiswahili fasaha.

e) Azingatie kwamba orodha ya vitabu vya kufundishia somo la Kiswahili vitakuwa vikitolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundi, na anaweza kutumia vitabu vya kiada zaidi ya kimoja.

f) Katika kidato cha tatu na nne, kila kidato kihakiki vitabu teule vya ushairi, tamthiliya na riwaya.

## 1.2 Muda wa Kufundishia

Muhtasari huu unafundishika kwa vipindi vitatu (3) kwa wiki. Kila kipindi kina dakika 40. Katika mwaka kuna siku 194 za masomo ambapo katika wiki kuna siku tano (5) za masomo. Kwa hiyo wiki za masomo ni 38.8 kwa mwaka. Mitihani huchukua wiki moja au zaidi kwa muhula. Hivyo wiki za masomo hubakia kuwa 36 tu kwa mwaka. Kwa kuwa kila wiki ina vipindi vitatu vya somo la Kiswahili, kwa mwaka kuna jumla ya vipindi 108. Vipindi hivi vimesambazwa katika kila mada kama inavyoonekana kwenye jedwali la ufundishaji na ujifunzaji. Usambazaji wake umezingatia urefu na ugumu wa mada.

## 2.0 Malengo ya Elimu Tanzania

Elimu itolewayo ni ya kurithisha maarifa, stadi na mielekeo bora toka vizazi vilivyopita kwa vizazi vya wakati huu na vijavyo. Hivyo yafuatayo ndiyo malengo ya elimu nchini:

a) Kuelekeza na kukuza maendeleo, kuboresha haiba ya wananchi wa Tanzania, rasilimali zao na matumizi bora ya rasilimali hizo katika kuleta maendeleo ya mtu binafsi na ya kitaifa;

b) Kukuza tabia ya kuthamini utamaduni, mila na desturi za watu wa Tanzania;

c) Kukuza upatikanaji wa fursa za kusoma, kuandika na kuhesabu na matumizi sahihi ya maarifa na stadi za kijamii, kisayansi, kiufundi, kiteknolojia, kitaalamu na aina nyingine za maarifa na ujuzi, kwa ajili ya maendeleo na kuboresha hali ya mtu na jamii;

d) Kukuza na kuendeleza kujiamini, kudadisi, weledi na kuheshimu utu wa mtu na haki za binadamu na kuwa tayari kufanya kazi kwa kujiendeleza na kwa maendeleo ya taifa.

e) Kuwezesha na kupanua mawanda ya kujipatia maarifa, kuboresha na kukuza stadi za kiakili, ki-vitendo, uzalishaji na nyinginezo zitakiwazo katika kukidhi mabadiliko ya ki-uchumi;

f) Kumwezesha kila raia kuelewa misingi ya katiba ya nchi pamoja na kuthamini haki za binadamu na uraia, wajibu na majukumu yanayoendana nayo;

g) Kukuza utashi wa kupenda na kuheshimu kazi za kujiajiri na kuajiriwa na kuboresha utendaji kazi katika sekta za uzalishaji na huduma;

h) Kujenga misingi ya maadili yanayokubalika kitaifa, ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na sheria kwa njia ya kujifunza;

i) Kuwezesha kuwapo kwa matumizi sahihi, usimamizi na utunzaji wa mazingira.

## 3.0 Madhumuni na Malengo ya Elimu ya Sekondari.

Nchini Tanzania elimu ya sekondari ni elimu rasmi inayotolewa kwa vijana waliomaliza darasa la saba na kupata sifa za kuingia sekondari. Hivyo malengo ya Elimu ya sekondari ni:

a) Kuimarisha na kupanua kina cha mawazo, maarifa, stadi na kanuni zilizo fundishwa na kukuzwa katika ngazi ya Elimu ya msingi.
b) Kuimarisha ukuaji na uthamini wa umoja utambulisho na maadili ya kitaifa, haiba, kuheshimu haki za binadamu, amali za kitamaduni, mila, desturi na wajibu wa kiraia na utayari wa kufanya kazi za kitaaluma na za mitulinga.
c) Kukuza umahiri wa lugha na kutumia stadi za mawasiliano katika Kiswahili na angalu lugha moja ya kigeni.
d) Kutoa fursa ya kupata maarifa, stadi, mielekeo na welewa katika nyanja teule za mafunzo.
e) Kuandaa wanafunzi kwa ajili ya elimu ya juu, elimu ya kazi, ufundi na taaluma.
f) Kuwajengea wanafunzi uwezo wa kujifunza, kujiamini, na tekinolojia, maarifa na stadi za kitaaluma na za kitaalamu.
g) Kuwaandaa wanafunzi kujiunga na ulimwengu wa kazi

## 4.0 Ujuzi wa Jumla wa Somo la Kiswahili

Wanafunzi wa sekondari wakijifunza somo la Kiswahili kwa kiwango cha kidato cha 1-4 watapata umahiri ufuatao.

a) Kusikiliza na kuwasiliana kwa Kiswahili katika miktadha mbalimbali.
b) Kukipenda na kukithamini Kiswahili kama lugha ya Taifa.
c) Kusoma maandiko mbalimbali ya Kiswahili kwa ufanisi.
d) Kuandika habari fupi na ndefu kwa Kiswahili sanifu.
e) Kusoma kwa ufahamu na burudani.
f) Kutumia lugha ya kifasihi katika mawasiliano kwa kuzingatia stadi zote za lugha.
g) Kutafiti vipengele mbalimbali vya Lugha ya Kiswahili.
h) Kuwasiliana kwa kutumia lugha ya ishara na alama (kwa viziwi).
i) Kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili kwa kutumia herufi za breili (kwa wasioona)

## 5.0 Malengo ya Jumla ya Kufundisha Somo la Kiswahili kwa Shule za Sekondari

Inatazamiwa kuwa mwanafunzi amalizapo elimu ya sekondari na kusoma somo la Kiswahili ataweza:

a) Kuwasiliana kwa Kiswahili fasaha katika fani mbalimbali za maisha.
b) Kukithamini Kiswahili kama ni sehemu muhimu ya utamaduni wa Tanzania.
c) Kujenga tabia ya udadisi na ubunifu katika masuala ya Lugha na Fasihi ya Kiswahili.
d) Kuelewa, kuthamini na kutumia kazi za fasihi katika maisha.
e) Kutumia lugha ya kisanii katika miktadha mbalimbali.
f) Kukuza na kukieneza Kiswahili ili kiweze kutumika kwa mawasiliano na nchi jirani na kimataifa.
g) Kujenga tabia ya kujisomea maandiko mbalimbali ya Kiswahili.
h) Kupata msingi bora na imara wa kujifunza na kujiendeleza.
i) Kutumia Kiswahili kupata maarifa, mwelekeo, na stadi za kijamii, kitamaduni, kiteknolojia na kitaaluma kutoka ndani na nje ya nchi.

## 6.0 Muundo wa Muhtasari

Muhtasari huu umeundwa na vipengele vifuatavyo:

a) Utangulizi
b) Malengo ya Elimu Tanzania
c) Malengo ya Elimu ya Sekondari
d) Umahiri wa jumla wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari
e) Malengo ya Jumla ya Kufundisha somo la Kiswahili katika shule za sekondari.
f) Umahiri, malengo na majedwali ya ufundishaji kidato cha 1 – 4.

## 7.0 Ufafanuzi wa vipengele vya muundo wa muhtasari wa kila kidato

### 7.1. Umahiri

Ni uwezo na stadi mwanafunzi atakaoupata baada ya kujifunza jambo fulani kwa muda maalum. Umahiri wa kila kidato umewekwa kabla ya malengo na majedwali ya kila kidato.

### 7.2 Malengo

Ni matarajio/mategemeo yanayotazamiwa kufikiwa na mwanafunzi baada ya kujifunza jambo fulani kwa muda maalum. Malengo ya kila kidato yapo mwanzoni mwa kila kidato baada ya umahiri wa kidato husika.

### 7.3 Mada kuu/ndogo

Safu hii inataja kwa kifupi maudhui yatakayoshughulikiwa. Mada kuu imeandikwa kwa herufi kubwa wakati mada ndogo imeonyeshwa kwa herufi mchanganyiko. Zingatia kuwa katika sehemu nyingi, mada ndogo kadhaa zimeonyeshwa na ndizo zinazojenga mada kuu.

### 7.4 Malengo mahususi

Safu hii inaonesha shughuli ambazo mwanafunzi ataweza kuzifanya baada ya kujifunza mada ndogo hiyo. Utendaji wa mwanafunzi katika safu hii ndio unaoonesha kwamba amejifunza na kuelewa.

### 7.5 Miundo

Hii ni safu ambayo inabeba maneno au viangama vya maneno vinavyotawala mpangilio wa maneno katika sentensi. Miundo hiyo huteuliwa kwa kuihusisha mada ndogo na malengo mahususi. Miundo hiyo hutakiwa kufundishwa wakati wa kufundisha mada ndogo inayohusika. Mwalimu atumie miundo hiyo kwa kuitungia sentensi kisha awatake wanafunzi watumie miundo hiyo katika miktadha mbalimbali.

### 7.6 Msamiati

Hii ni safu inayoonesha maneno yanayohusiana na mada hiyo ambayo hayajazoeleka kwa wanafunzi kwa kiwango chao. Maneno hayo yatatumika wakati wa kufundisha na kujifunza mada ndogo husika. Maneno hayo ni ya mifano tu. Mwalimu anatarajiwa aongeze mengine kulingana na mahitaji ya darasa lake.

### 7.7 Mbinu za kufundishia

Hii ni safu inayoonesha vitendo mbalimbali vya mwalimu na wanafunzi katika mchakato wa kujifunza.

**7.8 Zana/Vifaa**

Hii ni safu inayoonesha orodha ya vitu vinavyomsaidia mwalimu na wanafunzi katika kufikia malengo mahususi wakati wa kufundisha na kujifunza.

**7.9 Upimaji**

Hii ni safu yenye maswali inayomwongoza mwalimu kupima kama malengo mahususi yamefikiwa.

**7.10 Vipindi**

Hii ni safu inayoonesha idadi ya vipindi vinavyokadiriwa kutosheleza ufundishaji na ujifunzaji kwa kila mada kuu. Idadi iliyowekwa ni ya kukadiriwa tu. Mwalimu anaweza kurekebisha idadi hiyo kulingana na hali halisi ya wanafunzi wake na mazingira ya ufundishaji kwa ujumla.

## IDHINI

Elimu ya sekondari kidato cha I-IV ni kozi ya miaka minne ambayo imeandaliwa kwa ajili ya kumuandaa mwanafunzi kwa elimu ya sekondari ngazi ya juu yaani kidato cha sita, chuo cha ualimu au elimu ya juu. Mwanafunzi atatambulika kuwa na elimu ya kidato cha nne baada ya kuhitimu na kufaulu mitihani ya mwisho inayoandaliwa na Baraza la Mitihani Tanzania.

*Andiko hili limeidhinishwa kuwa ni* ***Muhtasari wa somo la Kiswahili*** *kidato cha I-IV kwa ngazi ya elimu ya chini ya sekondari.*

M. M. Wassena

Kamishna wa Elimu
**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**

## KIDATO CHA KWANZA

### UMAHIRI

Somo la Kiswahili kidato cha Kwanza linatazamiwa kumpatia mwanafunzi ujuzi wa:

1. Kuwasiliana kwa mazungumzo na maandishi kwa Kiswahili sanifu.
2. Kusoma na kuelewa maandiko mbalimbali ya Kiswahili.
3. Kusikiliza na kuelewa mazungumzo yaliyoko katika lugha ya Kiswahili
4. Kuandika habari fupi kwa kuzingatia taratibu za uandishi.
5. Kubainisha, kuhakiki na kutunga kazi za fasihi simulizi.
6. Kutumia kamusi.

### MALENGO

Inatazamiwa kwamba mwanafunzi amalizapo kidato cha kwanza ataweza:

(a) Kusikiliza na kuelewa taarifa au mazungumzo kwa Kiswahili yanayolingana na kiwango chake
(b) Kusoma na kuelewa maandiko na vitabu mbalimbali vya Kiswahili vyenye taarifa fupi na rahisi ili kupata ujumbe mahususi.
(c) Kuwasiliana kwa Kiswahili katika mazungumzo na maandishi na watu au jamii katika miktadha mbalimbali.
(d) Kujieleza kwa Kiswahili kwa kusimulia au kuandika habari fupi kwa kuzingatia taratibu za uandishi.
(e) Kubaini matumizi sahihi ya maneno katika tungo mbalimbali za Kiswahili
(f) Kubainisha, kuhakiki na kutunga kazi za fasihi simulizi kwa Kiswahili.
(g) Kutumia Kamusi
(h) Kujenga tabia ya kujisomea maandiko mbalimbali ya Kiswahili.

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1.0 MAWASILIANO**<br>1.1 Lugha kama Chombo cha Mawasiliano | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kueleza maana ya mawasiliano<br><br>b) Kufafanua dhima ya lugha katika mawasiliano | ..nge….nge<br>…kama….<br>..Kitambulisho…. | Mawasiliano, ufasaha | i) Kwa njia ya bunguabongo wanafunzi waeleze maana ya mawasiliano<br>ii) Wanafunzi wafanye mazoezi ya kuwasiliana bila kutumia lugha, kisha watumie lugha.<br>iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi wajadili maana ya lugha.<br>iv) Kwa kutumia maswali na majibu, pamoja na picha za mawazo mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili hali ingekuwaje kama binadamu asingekuwa na lugha.<br>v) Wanafunzi katika vikundi wajadili umuhimu wa lugha katika mawasiliano. | | Je, mwanafunzi ameweza:<br>1.Kueleza maana ya mawasiliano?<br><br>2. Kufafanua dhima ya lugha katika mawasiliano? | 4 |
| | c) Kueleza umuhimu wa kutumia lugha kwa ufasaha. | | | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili umuhimu wa kutumia lugha kwa ufasaha.<br>ii) Wanafunzi wajadili umuhimu wa kutumia lugha kwa ufasaha. | | 3. Kueleza umuhimu wa kutumia lugha kwa ufasaha? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.2 Matamshi na lafudhi ya Kiswahili. | Mwanafunzi aweze :<br>a) Kutofautisha kati ya matamshi sahihi na yasiyo sahihi ya Kiswahili<br><br>b) Kutumia matamshi na lafudhi sahihi ya Kiswahili. | | | i) Mwalimu aandike maneno kadhaa ubaoni kisha awaeleze wanafunzi wayatamke.<br>ii) Wanafunzi wayatamke kwa lafudhi na matamshi sahihi ya Kiswahili.<br>iii) Wanafunzi watofautishe kati ya matamshi sahihi na yasiyo sahihi ya Kiswahili<br>iv) Kwa kutumia dayalojia fupi mwalimu awaongoze wanafunzi kuigiza dayalojia wakizingatia matamshi na lafudhi sahihi ya Kiswahili. | Kanda za sauti, katuni zenye meneno yenye matamshi na lafudhi sahihi na isiyo sahihi. | 1. Je, mwanafunzi ameweza: Kutofautisha kati ya matamshi sahihi na yasiyo sahihi ya Kiswahili?<br><br>2.Kutumia matamshi na lafudhi sahihi ya Kiswahili? | 2 |
| **2.0 AINA ZA MANENO**<br>2.1 Ubainishaji wa Aina Saba za Maneno | Mwanafunzi aweze kubaini aina saba za maneno | Mtoto mzuri… …yule anaumwa ….. Ala! Kumbe! wewe! | Nomino, viwakilishi, vivumishi, vitenzi, | i) Kwa kutumia vitu halisi/ picha mwalimu awaelekeze wanafunzi watunge sentensi mbalimbali. | | | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Wameingia waume kwa wake .... wingi ...: ...lakini..... | vielezi, viunganishi, vihisishi. | ii) Wanafunzi watambue neno moja (nomino), kisha:<br>a) wafafanue dhima yake katika sentensi husika.<br>b) katika jozi wabaini maneno mengine yenye dhima kama hiyo katika sentensi nyingine.<br>iii) Kwa kutumia maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kufikia hitimisho la kundi la maneno kama hayo (nomino).<br>iv) Mwalimu atumie utaratibu huo kufundisha aina nyingine za maneno.<br>v) Wanafunzi wafanye mazoezi ya kubaini aina za maneno kwa kutumia matini, makala mbalimbali na chati ya sentensi. | i) Chati za ukutani za aina za maneno na ufafanuzi wake.<br>ii) Vitu halisi.<br>iii) Picha za vitu, watu na wanyama mbalimbali<br>iv) Chati ya sentensi mbalimbali. | Je Mwanafunzi ameweza kubaini aina saba za maneno? | 5 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.2 Ufafanuzi wa Aina Saba za Maneno. | Mwanafunzi aweze kufafanua kila aina ya neno. | Rushwa imetamalaki…<br>Ukimwi unaua…<br>….wengine wamefaulu…<br>….vyeupe …..<br>..alikuwa<br>….anafua …<br>…mara mbili...<br>…japokuwa…<br>..jamani!… | Nomino za: pekee, kawaida dhahania.<br>Viwakilishi: Vioneshi, Sifa, nafsi, ulinzi, milikishi, idadi amba, pekee, a-unganifu.<br>Vivumishi:- Sifa, vioneshi, ulinzi, milikishi, idadi, pekee, a-unganifu<br>Vitenzi:- Vikuu, visaidizi, vishirikishi.<br>Vielezi: sifa, namna, idadi wakati<br>Viunganishi.<br>Vihisishi. | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi watunge sentensi zenye nomino.<br>ii) Katika jozi wanafunzi:<br>a) wajadili dhima na sifa za nomino hizo.<br>b) wazipange nomino hizo katika makundi kulingana na sifa na dhima katika sentensi.<br>iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa maswali na majibu kufikia hitimisho la aina (tatu) za nomino.<br>iv) Mwalimu atumie utaratibu huu kufundishia aina za:- Viwakilishi, vivumishi, vitenzi, vielezi, viunganishi na vihisishi. | | Je mwanafunzi ameweza kufafanua kila aina ya neno? | 12 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.3 Matumizi ya Aina za Maneno katika Tungo | Mwanafunzi aweze kutumia aina saba za maneno kwa usahihi katika miktadha mbalimbali. | Kumbe!<br>….sikujua hilo!<br>Maji ni uhai… | | i) Mwalimu awaelekeze wanafunzi watunge sentensi mbalimbali kuonesha aina zote saba za maneno.<br>ii) Wanafunzi watunge sentensi hizo kwa mdomo na kwa kuandika. | | Je, mwanafunzi ameweza kutumia aina saba za maneno katika miktadha mbalimbali. | 4 |
| 2.4 Matumizi ya Kamusi | Mwanafunzi aweze kubaini maana za maneno kwa kutumia kamusi. | Maadili …. | Vidahizo, vitomeo, alfabeti kamusi | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi wachunguze mpangilio wa maneno katika kamusi.<br>ii) Kwa kutumia maswali na majibu wanafunzi waeleze mpangilio huo.<br>iii) Wanafunzi wajadili jinsi maneno yalivyofafanuliwa na kutolewa maana zake.<br>iv) Mwalimu awape wanafunzi mazoezi ya kutumia kamusi ili kupata maana za maneno. | Kamusi anuai<br>Chati ya alfabeti | Je mwanafunzi ameweza kutumia kamusi ili kupata maana za maneno? | 5 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **3.0 FASIHI KWA UJUMLA**<br><br>3.1 Dhima ya Fasihi | Mwanafunzi aweze kufafanua matumizi ya fasihi. | Kazi za kifasihi, ...kazi zisizo za kifasihi.<br><br>..umuhimu...<br>...dhima ya ..., | Fasili, sanaa, fasihi, hadhira, ujumbe. Hadithi, nyimbo, methali, mashairi vitendawili. | i) Kwa kutumia mifano ya kazi za kifasihi na zisizo za kifasihi mwalimu aongoze majadiliano ya vikundi kuhusu tofauti za kifani za kazi hizo.<br>ii) Wanafunzi wadadisi tofauti hizo na kuziwasilisha darasani.<br>iii) Mwalimu aongoze majadiliano na kufikia hitimisho la dhana ya fasihi.<br>iv) Mwalimu aongoze majadiliano ya matumizi na umuhimu wa kazi mbalimbali za Kifasihi katika jamii.<br>v) Kwa kutumia hadithi, nyimbo, methali na nahau wanafunzi wajadili katika jozi matumizi na umuhimu wa kazi za kifasihi katika jamii. | Chati ya methali, nahau, hadithi, vikato vya magazeti vyenye mashauri.<br><br>Vitabu na matini mbalimbali za kifasihi na zisizo za kifasihi | Je mwanafunzi ameweza kufafanua dhima ya fasihi? | 3 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 3.2 Aina za fasihi | Mwanafunzi aweza kufafanua aina za fasihi. | Aina za ...<br>fasihi simulizi<br>fasihi andishi | Usimulizi,<br>Uandishi. | i) Mwalimu aongoze majadiliano ya njia za uwasilishaji wa fasihi kwa kutumia masimulizi ya mdomo vitabu , kanda za nyimbo au maigizo vitabu.<br>ii) Wanafunzi washiriki katika majadiliano na kufikia hitimisho la njia za uwasilishaji wa kazi za kifasihi.<br>iii) Wanafunzi wakiongozwa na mwalimu wahusishe njia za uwasilishaji wa kazi za fasihi na aina za fasihi. | Kanda za nyimbo na maigizo, vitabu. | Je mwanafunzi ameweza kufafanua aina za fasihi? | 3 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **4.0 FASIHI SIMULIZI**<br>4.1. Ubainishaji wa Tanzu za Fasihi Simulizi | Mwanafunzi aweze:<br>Kubainisha tanzu za fasihi simulizi. | Fasihi simulizi …..<br>Tanzu za ….. | Tanzu, hadithi, ushairi, semi, maigizo. | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi waorodheshe kazi mbalimbali za kifasihi simulizi wanazozifahamu au wasikilize kanda za kazi za kifasihi simulizi.<br>ii) Wanafunzi wajadili maumbo ya kazi hizo na kuyaweka katika makundi ya mfanano.<br>iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kufikia hitimisho la tanzu za Fasihi Simulizi. | Kanda za sauti na video zenye kazi za fasihi simulizi | Je mwanafunzi ameweza kubainisha tanzu za fasihi? | 3 |
| 4.2. Ufafanuzi wa Vipera vya Tanzu za Fasihi Simulizi: | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kufafanua vipera vya hadithi | Vipera vya …<br>Hadithi….<br>Hadithi….<br>Paukwa….<br>Wakaishi raha mustarehe<br>Mwisho wa hadithi ….<br>Hapo zamani…. | Vipera vya hadithi:<br>hadithi soga ngano, vigano, visasili, tarihi, hekaya. | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasimulie hadithi mbalimbali.<br>ii) Wanafunzi wasimulie hadithi hizo. | Makala mbalimbali, magazeti, vitabu vya hadithi, kanda za sauti na video. | Je mwanafunzi ameweza kufafanua vipera vya hadithi? | 10 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | iii) Kwa kutumia maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi katika kivikundi kubaini vipera vya hadithi kwa kuzingatia maudhui yake.<br>iv) Mwalimu na wanafunzi wabainishe vipera vya hadithi kutokana na makundi ya mfanano. | | | |
| | b) Kufafanua vipera vya ushairi. | | Vipera vya ushairi:<br>- mashairi, tenzi, nyimbo, ngonjera.<br>- kutongoa, ghani. | i) Mwalimu na wanafunzi wakusanye kazi mbalimbali za ushairi au wasikilize kanda za sauti, video.<br>ii) Wanafunzi wazitongoe au kughani.<br>iii) Wanafunzi waziweke katika makundi yake kulingana na maumbo yake.<br>iv) Mwalimu awaongoze wanafunzi kufikia hitimisho kwa kuhusisha makundi hayo na vipera vya ushairi. | Kanda mbalimbali za sauti, video nyimbo, vitabu. | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua vipera vya ushairi? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | c) Kufafanua vipera vya semi | Malizia methali mtoto umleavyo .... <br> - tega kitendawili ... <br> - kitendawili ..tega mpe mji ..... <br> mkono wa birika. | Semi: Methali, misemo, nahau, mafumbo | i) Mwalimu awaelekeze wanafunzi wakusanye semi, methali, misemo au nahau. <br> ii) Wanafunzi katika vikundi wajadili na kuzipanga semi hizo kulingana na umbo, muundo na matumizi. <br> iii) Mwalimu awangoze wanafunzi kufikia hitimisho kwa kuhusisha makundi na vipera vya semi. | Mkusanyo wa semi, Methali, nahau, misemo, mafumbo. | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua vipera vya semi? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | d) Kufafanua vipera vya maigizo | ...kujigamba ..kutamba ..... mchezo wa kuigiza. | Maigizo: Vichekesho, michezo ya kuigiza, majigambo, ngonjera. | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasimulie aina mbalimbali za maigizo waliyowahi kuyaona kushiriki au wasikilize kanda.<br>ii) Wanafunzi wajadili na kuyapanga maigizo hayo katika makundi kulingana na utendekaji wake.<br>iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kufikia hitimisho kwa kuhusisha makundi hayo na vipera vya maigizo. | Kanda za sauti na video. | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua vipera vya maigizo?W | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 4.3. Uhakiki wa kazi za Fasihi simulizi | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kueleza umuhimu wa uhakiki wa kazi za fasihi simulizi. | .....kupima....<br>...kazi za fasihi ..... | Uhakiki, fani, maudhui, ubora, kufaa na kutokufaa, sadifu . | i) Wanafunzi wasimulie/ watongoe kazi yoyote ya Fasihi simulizi kwa zamu.<br>ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi watoe maoni yao kuhusu ubora wa kazi hizo kimaudhui na kifani.<br>iii) Kutokana na maoni hayo mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili umuhimu wa kutolea maoni kazi za kifasihi. | Matini za kazi za kifasihi, kanda za sauti. | Je mwanafunzi ameweza kueleza umuhimu wa uhakiki wa kazi za fasihi simulizi? | 10 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kufafanua vigezo vya uhakiki wa kazi za Fasihi Simulizi. | Kufaa au kutokufaa… ….kulingana na wakati …. faida kwa…... | Fani:- Wahusika, mandhari mtindo maudhui: Ujumbe, dhamira. | i) Mwalimu aongoze majadiliano kuhusu vigezo vinavyotumika kupima kazi za kifasihi simulizi.<br>ii) Wanafunzi kwa njia ya majadiliano wabaini vigezo vya kupima fasihi simulizi.<br>iii) Mwalimu ahitimishe vigezo vya uhakiki vya kifani na maudhui ambavyo ni muundo, mtindo, lugha, wahusika, mandhari, dhamira na ujumbe.<br>iv) Mwalimu asisitize umuhimu wa kutoa maoni ya kitathmini, yaani kufaa au kutokufaa kwake. | Matini za kazi za kifasihi, kanda za sauti na redio. | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua vigezo vya uhakiki wa kazi ya fasihi simulizi? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | d) kuhakiki matumizi ya semi katika fasihi simulizi. | Kwenda na wakati….<br>….usawa wa jinsia….. | Misemo, methali, nahau, mafumbo. | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wataje na waorodheshe semi mbalimbali.<br>ii) Wanafunzi wazipange katika vipera vyake.<br>iii) Mwalimu awangoze wanafunzi wabaini vigezo vya kifani na kimaudhui vya kazi za kifasihi za kila kipera wakizingatia kufaa au kutokufaa kwake.<br>iv) Wanafunzi wabaini vigezo vya kifani na kimaudhui vya kazi za kila kipera wakizingatia kufaa na kutofaa. | Matini za semi, methali, nahau, misemo | Je, mwanafunzi ameweza kuhakiki matumizi ya semi katika fasihi simulizi? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **5.0 USIMULIZI**<br>5.1 Usimulizi wa Hadithi | Mwanafunzi aweze kusimulia hadithi zenye maadili ya kijamii kwa kuzingatia Kiswahili fasaha. | Hadithi hadithi<br>Hapo zamani ..<br>Wakaishi … | Kiimbo, matamshi, utambaji, maadili. | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasimulie hadithi mbalimbali kutokana na uzoefu wao au kutoka kwenye matini alizosoma. Hadithi hizo zijumuishe zenye Elimu ya UKIMWI, Elimu ya Mazingira, Athari za ajira kwa watoto.<br>ii) Wanafunzi wajadili kufaa au kutofaa kwa habari hiyo.<br>iii) Kwa kila usimulizi wanafunzi wabaini na kusahihisha makosa ya kimatamshi, kiimbo na mbinu za utambaji.<br>iv) Wanafunzi wajadili kufaa au kutofaa kwa maadili ya hadithi hizo. | Picha kwenye mabango, vitini vyenye hadithi. | Je, mwanafunzi ameweza kusimulia hadithi kwa ufasaha? | 3 |
| 5.2 Usimulizi wa Habari | Mwanafunzi aweze kueleza habari kwa ufasaha. | Ajira ya mtoto | Ajira ,mtiririko | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasimulie habari au tukio kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili na mtiririko mzuri wa habari.<br>ii) Wanafunzi wajadili kufaa au kutofaa kwa habari hiyo. | | Je, mwanafunzi ameweza kueleza habari kwa ufasaha? | 4 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **6.0 UANDISHI WA INSHA**<br><br>Insha za Wasifu | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kueleza muundo wa insha | …aki… ata….<br>mtiririko wa….<br>mpangilio wa…<br>Insha za…. | Insha, wasifu, utangulizi, kiini, hitimisho, aya. | i) Mwalimu awape wanafunzi insha ambayo haina mtiririko mzuri wa mawazo.<br>ii) Mwalimu aongoze mwanafunzi mmoja mmoja katika jozi na katika vikundi wayapange mawazo hayo ili yalete mtiririko wa mantiki.<br>iii) Kwa kutumia insha hiyo, mwalimu atumie maswali na majibu kuwaongoza wanafunzi wabaini umbo la insha.<br>iv) Wanafunzi wajadili umbo hilo kwa kutumia chati ya umbo la insha. | Chati yenye muundo wa insha | Je, mwanafunzi ameweza kueleza muundo wa insha? | 10 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kutofautisha insha za kisanaa na zisizo za kisanaa. | Zisizo za …. …. za kisanaa | Utangulizi, kiini, Hitimisho. | i) Mwalimu alete darasani insha mbili kwenye mabango: moja ya kisanaa na nyingine isiyo ya kisanaa.<br>i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kubaini tofauti ya insha hizo kwa kutumia maswali na majibu na kwa majadiliano.<br>ii) Wanafunzi katika vikundi wajadili na kubaini tofauti hizo kwa kujibu maswali.<br>iii) Mwalimu aongoze majadiliano na wanafunzi kufikia hitimisho la sifa za insha za kisanaa na zisizo za kisanaa.<br>iv) Mwalimu aongoze majadiliano kuhusu matumizi ya aina zote za insha.<br>v) Wanafunzi katika vikundi wajadili matumizi ya aina za insha kwa mdomo na kwa maandishi. | Mabango ya insha, vitini vyenye insha. | Je, mwanafunzi ameweza kutofautisha Insha za kisanaa na zisizo za kisanaa? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| | c) Kuandika insha fupi za kisanaa na zisizo za kisanaa kwa kuzingatia taratibu za uandishi | Taratibu za uandishi….. Matumizi ya alama na vituo; herufi kubwa na ndogo. | - aya, nukta, mkato. | i) Kwa kutumia mifano mbalimbali ya insha mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili taratibu za uandishi wa insha.<br>ii) Kwa kutumia taratibu hizo mwalimu awaongoze wanafunzi waandike insha za kisanaa na zisizo za kisanaa kuhusu shughuli mbalimbali za kimaisha.<br>iii) Wanafunzi waandike insha za kisanaa na za kiada kuhusu shughuli mbalimbali za kimaisha. | Mifano mbalimbali ya insha. | Je, mwanafunzi ameweza kuandika insha za kisanaa na zisizo za kisanaa kwa kuzingatia taratibu za uandishi? | |
| **7.0 UANDISHI WA BARUA**<br><br>Barua za Kirafiki | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kueleza muundo wa barua za kirafiki. | Muundo wa barua za Mpendwa …., Mwanzo wa… Kiini cha ….. Mwisho wa…. Jina la mwandishi. Salam sana | Barua, maamkizi, kiini, maagano, wasalam. | i) Mwalimu na wanafunzi walete barua za kirafiki na wazisome darasani.<br>ii) Mwalimu aongoze majadiliano ya vikundi kubaini muundo wa barua kwa kutumia barua chache zilizosomwa.<br>iii) Wanafunzi wajadili na kubaini muundo wa barua zilizosomwa. | Barua za kirafiki zilizopokewa. | Je, mwanafunzi ameweza kueleza muundo wa barua za kirafiki? | 7 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kuandika barua za kirafiki. | Taratibu za….<br>Matumizi ya… | Aya, pambizo. | i) Kwa kutumia barua zilizoletwa darasani mwalimu awaongoze wanafunzi katika jozi wahakiki na kutoa maoni yao kuhusu taratibu za uandishi katika barua walizoleta.<br>ii) Wanafunzi katika vikundi wajadili na kutoa maoni yao kuhusu taratibu za uandishi wa barua za kirafiki.<br>iii) Kwa kutumia oneshombinu mwalimu awangoze wanafunzi kuandika barua za kirafiki.<br>iv) Wanafunzi waandike barua za kirafiki kwa kuzingatia muundo na taratibu za uandishi. | Barua zilizokwisha andikwa | Je, mwanafunzi ameweza kuandika barua za kirafiki kwa kuzingatia muundo na taratibu za uandishi? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | c) Kuandika jina na anuani juu ya bahasha.<br><br>d) Kufafanua njia mbalimbali za kutuma barua. | Uandishi wa anuani juu ya ……<br>Sanduku la pekee …..<br>…. Kwa mkono<br>….. kwa posta.<br>S.L.P | - Posta, (stempu),<br>- nukushi,<br>- Bahasha. | i) Wanafunzi walete bahasha zilizotumika kubebea barua.<br>ii) Katika vikundi wanafunzi wachunguze taratibu za uandishi wa jina la mpelekewa na anuani juu ya bahasha hizo.<br>iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili na kuhitimisha taratibu za uandishi wa jina la mpelekewa na anuani juu ya bahasha.<br>iv) Mwalimu na wanafunzi wajadili njia mbalimbali za kutuma barua. | Bahasha zilizotumika na zisizotumika, stempu | Je, mwanafunzi ameweza:<br>1. Kuandika jina na anuani juu ya bahasha kwa kufuata taratibu za uandishi?<br><br>2. Kufafanua njia mbalimbali za kutuma barua. | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **8.0 UFAHAMU**<br>8.1 Kusikiliza | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kujibu maswali kutokana na habari aliyoisikiliza. | ...kwa makini<br>...kuwa makini.... | Makini, usikivu, uelewa, utulivu. | i) Mwalimu asome kwa ufasaha matini/ makala kulingana na kiwango cha darasa.<br>ii) Wanafunzi wasikilize kwa makini.<br>iii) Mwalimu awaulize wanafunzi maswali ya kufikirisha, kumbukumbu na ya uhakiki kutokana na habari waliyoisikiliza.<br>iv) Wanafunzi wajadili kisha wajibu maswali hayo kwa mdomo na kwa kuandika. | Makala ya masuala ya Jinsia, Ukimwi, madawa ya kulevyaa na ajira ya watoto. | Je, mwanafunzi ameweza kujibu maswali kutokana na habari aliyosikiliza? | 5 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | a) Kufupisha habari | Kiini cha habari, mtiririko wa mawazo... kichwa cha habari. | Kiini, mantiki | i) Wanafunzi wakiongozwa na mwalimu wabaini mawazo makuu kutokana na habari waliyoisikiliza.<br>ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi wafupishe habari hiyo kwa kuunganisha mawazo makuu na kufuata taratibu za ufupisho.<br>iii) Wanafunzi wafupishe habari waliyoisikiliza kwa maneno yasiyozidi theluthi moja. | Matini zenye habari na ufupisho wake. | Je, mwanafunzi ameweza kufupisha habari aliyoisikiliza? | |
| 8.2 Kusoma kwa Sauti | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kusoma kwa sauti kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili. | .... kwa sauti | Viimbo, lafudhi, matamshi, usikivu. | i) Mwanafunzi mmoja asome habari kwa sauti.<br>ii) Mwalimu aongoze majadiliano kuhusu usomaji ule kwa kuzingatia kiimbo, matamshi na sauti.<br>iii) Wanafunzi wasome matini mbalimbali katika makundi na kusahihisha na wakizingatia lafudhi na sauti. | Makala, matini na vitabu mbalimbali zikiwemo zenye masuala ya UKIMWI, Ajira ya watoto, Jinsia na madawa ya kulevya. | Je, mwanafunzi ameweza kusoma kwa sauti kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili? | 6 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kujibu maswali kutokana na habari aliyoisoma. | | | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi- mmoja mmoja na kwa vikundi, wajibu maswali ya ufahamu.<br>ii) Wanafunzi wajibu maswali, wafupishe habari na kueleza habari kwa maneno yao wenyewe. | | Je, mwanafunzi ameweza kujibu maswali ya habari aliyoisoma kwa sauti? | |
| 8.3 Kusoma kimya | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kujibu maswali kutokana na habari waliyosoma. | Kasi ya usomaji | | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome kimya makala/matini mbalimbali zikiwemo zenye masuala ya kilimo, biashara na ufugaji.<br>ii) Mwalimu awape maswali kutokana na habari waliyoisoma.<br>iii) Wanafunzi wajadili maswali hayo katika vikundi kisha wajibu kwa kuandika au kuzungumza. | Matini zenye habari/ makala mbalimbali, vitabu. | Je, mwanafunzi ameweza kujibu maswali kutokana na habari aliyoisoma? | 7 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kufupisha habari aliyosoma. | Soma kimya... | | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wabaini mawazo makuu kutokana na habari waliyoisoma.<br>ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi wafupishe habari hiyo kwa kuunganisha mawazo makuu kwa kuzingatia taratibu za ufupisho.<br>iii) Wanafunzi wafupishe habari waliyosoma kwa maneno yasiyozidi theluthi moja. | | Je, mwanafunzi ameweza kufupisha habari aliyoisoma kwa kuzingatia taratibu za ufupisho? | |
| 8.4 Kusoma kwa Burudani | a) Mwanafunzi aweze kusoma kwa burudani | Kusoma kwa burudani<br>Jina la kitabu | Mwandishi<br>mchapishaji | i) Wanafunzi wasome vitabu au matini wanazozipenda.<br>ii) Mwalimu aweke rekodi za kumbukumbu za usomaji wa wanafunzi. | Vitabu, matini, makala mbalimbali zikijumuisha masuala ya Ukimwi, jinsia, ajira mbaya ya mtoto. | Je, mwanafunzi ameweza kusoma kwa burudani? | 5 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kutoa taarifa ya kila kitabu alichosoma. | | | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi watoe taarifa kuhusu vitabu au matini walizosoma akizingatia fani na maudhui, pia jina la kitabu, mchapishaji, mwandishi na mhariri.<br>ii) Wanafunzi watoe taarifa kuhusu vitabu au matini walizosoma wakizingatia vipengele vya fani na maudhui jina la kitabu au matini, mchapishaji, mwandishi na mhariri kwa mdomo na kwa kuandika. | | Je, mwanafunzi ameweza kutoa taarifa sahihi ya kila kitabu alichokisoma? | |

## KIDATO CHA PILI

### UMAHIRI

Somo la Kiswahili katika kidato cha pili linatazamiwa kumpatia mwanafunzi ujuzi ufuatao:

1. Kusikiliza na kuelewa mazungumzo yaliyo katika lugha ya Kiswahili.
2. Kuzungumza na kuandika kwa Kiswahili.
3. Kusoma na kuelewa habari fupifupi za Kiswahili.
4. Kuandika habari fupifupi za Kiswahili.
5. Kubainisha na kutunga kazi za Fasihi Simulizi.
6. Kukusanya na kuhifadhi kazi za Fasihi Simulizi.
7. Kuhakiki kazi za Fasihi Simulizi.

### MALENGO

Inatazamiwa kwamba mwanafunzi amalizapo kidato cha pili ataweza:

(a) Kutumia maneno kwa ufasaha.
(b) Kubainisha matumizi ya Kiswahili katika miktadha mbalimbali.
(c) Kutunga na kuhakiki kazi za kifasihi simulizi
(d) Kukusanya na kuhifadhi kazi za kifasihi simulizi
(e) Kuandika insha, barua na simu
(f) Kusoma na kuelewa maandiko yenye ujumbe mbalimbali
(g) Kusikiliza na kuelewa masimulizi mbalimbali atakayosimuliwa.

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1.0 UUNDAJI WA MANENO**<br><br>1.1 Kutumia Uambishaji | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kubainisha mofimu katika maneno. | | mofimu, kipashio kiambishi`. | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wataje vitenzi kadhaa.<br>ii) Wanafunzi wavitaje na mwalimu aviandike ubaoni.<br>iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kubadili vipashio mwanzoni na mwishoni mwa maneno hayo.<br>iv) Wanafunzi wabaini mabadiliko ya maana kutokana na mabadiliko ya viambishi.<br>v) Mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa fasili ya mofimu.<br>vi) Wanafunzi wafanye mazoezi ya kubadili maana za maneno kwa kubadilisha mofimu. | Chati za ukutani zinazoonesha viambishi kwenye maneno. | Je, mwanafunzi ameweza kueleza maana ya mofimu? | 5 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kufafanua dhima za mofimu | mofimu huru mofimu tegemezi, mofimu za/ ya... | | i) Mwalimu atumie njia ya maswali na majibu kuwaongoza wanafunzi wafafanue dhima za mofimu.<br>ii) Wanafunzi wataje maneno kadhaa, kisha kwa njia ya majadiliano wabainishe mofimu za kila neno na dhima zake.<br>iii) Wanafunzi wakiongozwa na mwalimu wataje maneno mbalimbali kisha wajadili na kubaini mofimu tegemezi na mofimu huru katika maneno hayo.<br>iv) Wanafunzi watumie mofimu mbalimbali katika kuunda maneno.<br>v) Wanafunzi watumie maneno hayo katika sentensi. | | Je, mwanafunzi ameweza kutaja aina za mofimu? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.2 Kutumia Mnyumbuliko | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kueleza mazingira yanayosababisha mahitaji ya maneno mapya. | | Ngamizi, sasisha, habarisha, katiana, | i) Mwalimu atumie maswali na majibu na majadiliano kuibua fikra za wanafunzi kuhusu miktadha inayodai matumizi ya maneno mapya.<br>ii) Wanafunzi wajadili na kueleza miktadha inayohitaji matumiziya maneno mapya. Miktadha hiyo ijumuishe teknolojia, sanaa na sayansi. | Chati za ukutani zinazoonesha viambishi kwenye maneno. | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua mazingira yanayosababisha mahitaji ya maneno mapya? | 5 |
| | b) Kufafanua dhima ya uambishaji na mnyumbuliko wa maneno. | | Uambishaji, mnyumbuliko, nyumbulisha | i) Mwalimu atumie mifano, maswali na majibu na majadiliano katika kufafanua maana na dhima ya uambishaji na mnyumbuliko wa maneno.<br>ii) Wanafunzi wajibu maswali yanayohusu maana na dhima ya uambishaji na mnyumbuliko wa maneno. | | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua maana na dhima ya uambishaji na mnyumbuliko wa maneno? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | c) Kuunda maneno mbalimbali kwa kutumia mnyumbuliko | | miktadha | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi waunde maneno mbalimbali kwa kutumia mnyumbuliko.<br>ii) Wanafunzi wafanye mazoezi ya kuunda maneno mbalimbali kwa kutumia mnyumbuliko. | Picha za katuni za dhima za mnyumbuliko | Je, mwanafunzi ameweza kuunda maneno mbalimbali kwa kutumia mnyumbuliko? | |
| | d) Kutumia maneno ya mnyumbuliko katika miktadha mbalimbali | | | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi watunge sentensi kwa kutumia maneno ya mnyumbuliko.<br>ii) Wanafunzi watumie maneno hayo katika miktadha mbalimbali ikijumuisha masuala ya Ukimwi, Jinsia, Kilimo, Elimu ya Mazingira. | | Je, mwanafunzi ameweza kutumia maneno katika miktadha mbalimbali? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **2.0 MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MIKTADHA MBALIMBALI**<br><br>2.1. Rejesta | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kuwasiliana kwa kutumia rejesta. | Bei gani….<br>Nani kuku…<br>…wali ng'ombe;<br>…pisha mzinga; | Rejesta, dhima mahakama, gulio, dalali, kuli, mgahawa, bandari, mshtakiwa. | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika maigizo ya kutumia rejesta katika mazingira mbalimbali hotelini, gulioni, mahakamani.<br>ii) Wanafunzi washiriki katika maigizo kisha wajadili kuhusu fasili na dhima ya rejesta.<br>iii) Kwa kutumia bungua bongo mwalimu awaongoze wanafunzi wataje rejesta zinazotumika katika miktadha mbalimbali.<br>iv) Mwalimu awaongoze wanafunzi wafanye kazi mradi ya kukusanya rejesta zinazotumika katika mazingira mbalimbali.<br>v) Kazi mradi hizo ziwasilishwe darasani ili zijadiliwe na kutolewa maoni. | Matini zenye rejesta. | Je, mwanafunzi ameweza kuwasiliana kwa kutumia rejesta? | 5 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| 2.2. Misimu | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kuwasiliana kwa kutumia misimu | Oyaa!! Hamna noma…. Weka, toa kiwingu… utajiju… mambo… poa | Misimu, teja, mshikaji | i) Mwalimu atoe mifano kadhaa ya misimu na wanafunzi waeleze chanzo; sababu na matumizi ya misimu hiyo.<br>ii) Wanafunzi watoe misimu wanayoijua kisha waeleze umuhimu na matumizi yake.<br>iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi wafanye kazi mradi za kukusanya misimu inayotumika katika miktadha mbalimbali.<br>iv) Wanafunzi wazilete kazi hizo darasani kisha wazijadili katika vikundi. | Vitini vya misimu | Je, mwanafunzi ameweza kutumia misimu katika kuwasiliana? | 3 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.3.<br>Lugha ya Kimazungumzo na ya Kimaandishi | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kubainisha sifa za lugha ya kimazungumzo na ya kimaandishi. | … tofauti baina ya<br>…..<br>lugha ya….<br>… wasiliana kwa…<br>… ya | Kubainisha, lugha. | i) Mwalimu awasomee wanafunzi matini yenye kutumia lugha ya kimazungumzo na yenye lugha ya kimaandishi.<br>ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi wazichunguze na kujadili ili kubaini tofauti ya mtindo wa lugha ya kimazungumzo na lugha ya kimaandishi.<br>iii) Wanafunzi wajadili tofauti za lugha ya kimazungumzo na kimaandishi. | Vitini vya lugha ya | Je, mwanafunzi ameweza kubainisha sifa za lugha ya kimazungumzo na ya kimaandishi? | 4 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kueleza dhima ya lugha ya kimazungumzo na ya kimaandishi. | | Hadithia, elezea | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya maswali na majibu kueleza dhima ya lugha ya kimazungumzo na ya kimaandishi.<br>ii) Wanafunzi wajadiliane na wajibu maswali katika kueleza dhima ya lugha ya mazungumzo na ya maandishi. | | Je, mwanafunzi ameweza kueleza dhima ya lugha ya mazungumzo na ya maandishi? | |
| | c) Kutumia lugha ya kimazungumzo na ya kimaandishi katika miktadha sahihi. | | | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi watumie lugha ya kimazungumzo na ya kimaandishi katika miktadha sahihi.<br>ii) Wanafunzi kivikundi wafanye mazoezi ya kutumia lugha ya mazungumzo na ya maandishi katika miktadha sahihi. | Vikatuni vyenye mazungumzo | Je, mwanafunzi ameweza kutumia lugha ya kimazungumzo na ya maandishi katika miktadha sahihi? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.4 Matamshi na Lafudhi ya Kiswahili | Mwanafunzi aweze kutumia matamshi na lafudhi sahihi ya Kiswahili katika kuwasiliana. | | | i) Mwalimu na wanafunzi wasikilize kanda za sauti zenye mazungumzo ya mchanganyiko yenye matamshi na lafudhi sahihi ya Kiswahili.<br><br>ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi kubaini mazungumzo ya matamshi na lafudhi sahihi ya Kiswahili.<br>iii) Wanafunzi wajadili na kubaini tofauti hizo wakizingatia matamshi na lafudhi sahihi ya Kiswahili. | Kanda za sauti zenye mazungumzo | Je, mwanafunzi ameweza kutumia matamshi na lafudhi sahihi ya Kiswahili katika kuwasiliana. | 3 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.5 Utata katika Mawasiliano | Mwanafunzi aweze kubaini maana tofauti zinazopatikana kutokana na matumizi ya maneno yenye maana zaidi ya moja. | ..utata katika … | tata…. miktadha. | i) Mwalimu awape wanafunzi tungo kadhaa zilizoundwa na maneno yenye maana zaidi ya moja.<br>ii) Wanafunzi wajadili maana tofauti zinazopatikana katika sentensi hizo na sababu zake.<br>iii) Kwa kila sentensi wanafunzi katika vikundi wajadili jinsi ya kuondoa utata huo. | Bango lenye tungo zenye maneno yenye maana zaidi ya moja. | Je, mwanafunzi ameweza kubaini tofauti zinazopatikana kutokana na matumizi ya maneno yenye maana zaidi ya moja? | 3 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **3.0 UHAKIKI WA KAZI ZA KIFASIHI SIMULIZI**<br><br>3.1 Uhakiki wa ushairi | Mwanafunzi aweze kuhakiki kazi za ushairi katika fasihi simulizi. | Mbinu za kifani | Fani:- Matumizi ya lugha, wahusika, miundo, mitindo | i) Kwa kutumia matini za ushairi, kanda, kinasa sauti mwalimu aongoze majadiliano ya kubaini vepengele vya maudhui ya kazi za kishairi katika fasihi simulizi.<br>ii) Wanafunzi wajadili kufaa au kutokufaa kwa vipengele hivyo wakizingatia hali halisi ya jamii.<br>iii) Mwalimu aongoze majadiliano kuhusu vipengele vya fani katika ushairi wa fasihi simulizi.<br>iv) Wanafunzi wajadili kufaa au kutokufaa kwa vipengele hivyo wakizingatia hali halisi ya jamii kwa mdomo na kwa kuandika. | Matini za ushairi, kinasa sauti na kanda zake. | Je mwanafunzi ameweza kuhakiki maudhui na fani ya kazi ya ushairi katika fasihi simulizi? | 12 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 3.2. Uhakiki wa Maigizo | Mwanafunzi aweze kuhakiki maigizo. | | Igizo, fanani, hadhira, mgogoro. | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi waigize maigizo au wasikilize kanda.<br>ii) Kwa kutumia maigizo mwalimu aongoze majadiliano ya kubaini vipengele vya maudhui ya maigizo.<br>iii) Wanafunzi wajadili kufaa au kutofaa kwa vipengele hivyo wakizingatia hali halisi ya jamii.<br>iv) Mwalimu aongoze majadiliano ya kubaini vipengele vya fani katika maigizo.<br>v) Wanafunzi wajadili kufaa au kutofaa kwa vipengele hivyo wakizingatia hali halisi ya jamii kwa mdomo na kwa kuandika. | Matini za maigizo, kinasa sauti na kanda zake. | Je mwanafunzi ameweza kuhakiki maudhui na fani katika maigizo? | 9 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **4.0 UHIFADHI WA KAZI ZA KIFASIHI SIMULIZI**<br><br>4.1 Njia za Kuhifadhi Fasihi Simulizi | Mwanafunzi aweze:<br>a) kubainisha njia za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi<br>b) Kueleza ubora na udhaifu wa kila njia ya kuhifadhi kazi za fasihi simulizi. | Uhifadhi wa…..<br>Njia za/ ya…. | Kanda, sauti. | i) Kwa kutumia vitabu, vinasa sauti kanda mbalimbali mwalimu awaongoze wanafunzi wabaini njia mbalimbali, za kuhifadhia kazi za kifasihi simulizi.<br>ii) Wanafunzi wataje njia mbalimbali za kuhifadhi kazi za kifasihi simulizi.<br>iii) Wanafunzi wajadili ubora na udhaifu wa kila njia za kuhifadhi kazi za kifasihi simulizi. | Vinasa sauti na kaseti zake. | Je mwanafunzi ameweza:<br>Kubainisha njia za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi?<br><br>Kueleza ubora na udhaifu wa kila njia ya kuhifadhi kazi za fasihi simulizi? | 3 |
| 4.2. Umuhimu wa Kuhifadhi Kazi za Fasihi Simulizi | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kueleza umuhimu wa kuhifadhi kazi za kifasihi simulizi. | | | i) Mwalimu aongoze majadiliano kuhusu umuhimu wa kuhifadhi kazi za kifasihi simulizi.<br>ii) Wanafunzi wabainishe umuhimu wa kuhifadhi fasihi simulizi. | | Je mwanafunzi ameweza kueleza umuhimu wa kuhifadhi kazi za fasihi simulizi? | 2 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kuhifadhi kazi za fasihi simulizi. | | | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wakusanye na wasimulie kazi za ushairi na maigizo.<br>ii) Wanafunzi wachague kipera kimoja katika utanzu wa ushairi au maigizo wahifadhi kwa kutumia njia mbalimbali. | Vinasa sauti, nukuu, kaseti | Je mwanafunzi ameweza kuhifadhi kazi za fasihi simulizi? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **5.0 UTUNGAJI WA KAZI ZA KIFASIHI SIMULIZI**<br><br>5.1 Kanuni za utungaji wa mashairi. | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kutunga mashairi kwa kuzingatia kanuni. | …. urari wa vina na mizani. | Mizani, vina, urari, bahari, mapokeo, kanuni, sheria... kituo, ubeti, tamba. | i) Wanafunzi walete kazi mbalimbali za ushairi. zikiwemo mashairi, tenzi, nyimbo.<br>ii) Wanafunzi waimbe, wasome, na watongoe kazi mbalimbali za ushairi.<br>iii) Wanafunzi wazichunguze kisha katika vikundi wajadili na wabaini kanuni mbalimbali zilizotumika katika utungaji wa kazi hizo.<br>iv) Mwalimu atumie onesho mbinu kuonesha hatua za utungaji wa mashairi, ngonjera, tenzi.<br>v) Wanafunzi wafanye mazoezi ya kutunga kazi za ushairi wazingatie masuala ya UKIMWI, jinsia, kilimo, ajira ya watoto, madawa ya kulevya. | Matini mbalimbali za mashairi, tenzi, ngongera. | Je mwanafunzi ameweza kutunga mashairi kwa kuzingatia kanuni? | 8 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kuigiza ngonjera | Uigizaji wa ……<br>…kwa madaha… | Ngonjera, biashara, kutamba | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma na kukariri ngonjera.<br>ii) Wanafunzi waigize ngonjera walizozikariri. | | Je mwanafunzi ameweza kuigiza ngonjera? | |
| 5.2. Maigizo | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kueleza taratibu za kutunga maigizo. | ..mtiririko wa matukio | Mtiririko, visa. | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wafanye maigizo mbalimbali yakiwemo yenye masuala ya UKIMWI, Jinsia, maadili ya Jamii na Ajira ya Watoto.<br>ii) Wanafunzi wafanye maigizo hayo.<br>iii) Mwalimu aongoze wanafunzi wajadili taratibu za utungaji wa maigizo.<br>iv) Wanafunzi wajadiliane na kubaini mbinu za utungaji wa maigizo. | Matini za maigizo | Je mwanafunzi ameweza kueleza taratibu za kutunga maigizo? | 7 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kutunga maigizo. | Maigizo ya….. | | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kutunga maigizo.<br>ii) Wanafunzi watunge maigizo wakizingatia masuala ya jinsia, madawa ya kulevya, Ukimwi. | | Je mwanafunzi ameweza kutunga maigizo? | 5 |
| **6.0 UANDISHI**<br>6.1 Insha za Hoja | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kubaini mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha za hoja. | …hoja …..<br>... pinga hoja..<br>…jenga hoja..<br>… mtiririko wa mawazo. | hoja | i) Mwalimu kwa kutumia matini zenye insha za hoja awaongoze wanafunzi kubaini taratibu za uandishi wa insha za hoja.<br>ii) Wanafunzi kivikundi washiriki katika majadiliano kubaini taratibu za uandishi wa insha za hoja | Matini, zenye, insha za hoja. | Je mwanafunzi ameweza kubaini mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha za hoja? | |
| | b) Kuandika insha fupi za hoja kwa kuzingatia taratibu za uandishi. | | …lugha sanifu… | i) Mwalimu awape wanafunzi mazoezi ya kuandika insha fupi za hoja kwa kuzingatia taratibu za uandishi.<br>ii) Wanafunzi waandike insha fupi za hoja kwa kuzingatia taratibu za uandishi. | | Je mwanafunzi ameweza kuandika insha fupi za hoja kwa kuzingatia taratibu za uandishi? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 6.2 Barua Rasmi | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kueleza dhima ya barua rasmi. | …pasha habari …<br>…jibu barua... | Taarifa haraka mawasiliano. | i) Mwalimu na wanafunzi wakusanye na kuzileta darasani barua rasmi zilizopokewa.<br>ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome barua zilizoletwa darasani.<br>iii) Kwa kutumia majadiliano ya vikundi wanafunzi wajadili dhima ya barua rasmi. | Barua rasmi | Je mwanafunzi ameweza kueleza dhima ya barua rasmi? | 5 |
| | b) Kuandika barua rasmi kwa kufuata taratibu za uandishi. | …<br>namba ya | Rasmi, saini | i) Wanafunzi wakiongozwa na mwalimu wachunguze barua zilizoletwa, kisha wajadili na kubaini muundo na taratibu zilizotumika katika uandishi wa barua hizo.<br>ii) Wanafunzi waandike barua rasmi kwa kufuata taratibu za uandishi. | | Je mwanafunzi ameweza kuandika barua rasmi? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 6.3. Simu | Mwanafunzi aweze:-<br>a) Kueleza dhima ya simu ya maandishi. | Tuma simu jibu simu … taarifa ya simu | haraka, muhtasari. | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome baadhi ya simu za maandishi zilizoandaliwa.<br><br>ii) Kwa kutumia majadiliano mwalimu awaongoze wanafunzi wajadili dhima za simu za maandishi.<br>iii) Wanafunzi katika vikundi wajadili dhima za simu za maandishi. | Simu zilizopokewa | Je mwanafunzi ameweza kueleza dhima ya simu ya maandishi? | 5 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kuandika simu za maandishi kwa kuzingatia muundo na taratibu za uandishi. | kuandika simu, ... ni njia haraka ... kwa maneno | Simu | i) Wanafunzi katika vikundi wachunguze baadhi ya simu za maandishi zilizoletwa kisha wajadili muundo na taratibu za uandishi wa simu.<br>ii) Wanafunzi wafanye mazoezi ya kuandika simu za maandishi.<br>iii) Wanafunzi, kulingana na uzoefu wao, wataje matumizi ya simu za maandishi. | | Je mwanafunzi ameweza kaundika simu za maandishi? | |
| 6.4. Kadi za Mialiko | Mwanafunzi aweze kuandika kadi za mialiko. | Bwana na Bi/Bibi..... Ndugu..... Kadi ya..... | alika, kadi. | i) Mwalimu na wanafunzi wakusanye na walete darasani kadi za mialiko mbalimbali.<br>ii) Mwalimu katika vikundi awaongoze wanafunzi wachunguze kadi za mialiko mbalimbali | Kadi za mialiko mbalimbali. | Je mwanafunzi ameweza kuandika kadi za mialiko? | 5 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | iii) Wanafunzi kivikundi wajadili na kubaini muundo na taratibu za uandishi wa kadi za mialiko.<br>iv) Wanafunzi waandike kadi za mialiko mbalimbali wakizingatia taratibu na muundo. | | | 5 |
| 6.5 Uandishi wa Dayalojia | Mwanafunzi aweze Kuandika dayalojia | …kwa zamu<br>…kwa kupokezana | dayalojia, pokezana. | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome dayalojia mbalimbali.<br>ii) Wanafunzi wasome na kuigiza dayalojia, zikiwamo zenye masuala ya Ukimwi, Jinsia, Madawa ya Kulevya, Elimu ya Mazingira. | Picha mabango | Je mwanafunzi ameweza kuandika dayalojia? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | muhusika | iii) Mwalimu awape wanafunzi matini za dayalojia.<br>iv) Wanafunzi katika vikundi wachunguze na kujadili mbinu zilizotumika katika kuandika dayalojia hizo.<br>v) Wanafunzi wafanye mazoezi ya kuandika dayalojia. | Matini zenye dayalojia. | | 2 |
| **7.0 USIMULIZI**<br><br>Usimuliaji wa Matukio | Mwanafunzi aweze kusimulia matukio mbalimbali kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili. | …ilikuwa<br>….<br>…sitasahau<br>…<br>…<br>kupanda na | Lafudhi | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi mmoja mmoja wasimulie matukio mbalimbali yaliyotokea katika maeneo yao wakizingatia lafudhi ya Kiswahili.<br>ii) Wanafunzi wasimulie matukio mbalimbali kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili. | Magazeti, mabango, matangazo | Je mwanafunzi ameweza kusimulia matukio mbalimbali kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **8.0 UFAHAMU**<br>8.1 Ufahamu wa Kusikiliza | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kujibu maswali ya ufahamu kutokana na habari aliyoisikiliza. | | | i) Mwalimu asome habari iliyoandaliwa kwa ufasaha.<br>ii) Wanafunzi wasikilize kwa makini habari inayosomwa.<br>iii) Mwalimu awape wanafunzi maswali ya ufahamu kutokana na habari waliyosikiliza.<br>iv) Wanafunzi wajibu maswali hayo kwa kusema au kuandika. | Vitabu, maandiko mbalimbali | Je mwanafunzi ameweza kuonesha ufahamu wa habari aliyoisikiliza? | 4 |
| | b) Kufupisha kwa mdomo habari aliyoisikiliza. | | ufupisho | i) Mwalimu awape wanafunzi mazoezi ya kufupisha kwa mdomo habari waliyoisikiliza.<br>ii) Wanafunzi wafanye mazoezi ya kufuipisha kwa mdomo habari waliyoisikiliza. | Vitabu, matini mbalimbali, mabango | Je mwanafunzi ameweza kufupisha kwa mdomo habari aliyoisikiliza? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 8.2 Ufahamu wa Kusoma | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kusoma kwa sauti kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili. | …kwa sauti… | Matamshi, makini, | i) Mwalimu aongoze onesho mbinu la kusoma kwa sauti kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili.<br>ii) Wanafunzi wafanye mazoezi ya kusoma kwa sauti matini mbalimbali/ vitabu kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili. | Maandiko mbalimbali pamoja na yale yenye masuala mtambuko. | Je mwanafunzi ameweza kusoma kwa sauti kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili. | 8 |
| | b) Kujibu maswali kutokana na habari waliyosoma. | | | i) Mwalimu aandae maswali yanayofikirisha ya kuonesha welewa.<br>ii) Wanafunzi, mmoja mmoja na katika vikundi wajibu maswali na kueleza habari kwa maneno yao. | | Je, mwanafunzi ameweza kuonesha welewa kwa kujibu maswali ya habari waliyoisoma? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | c) Kujibu maswali kutokana na habari aliyoisoma kimya. | …muda wa kusoma<br>…kwa kasi<br>…kwa utulivu… | kasi | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wasome habari kimya kwa muda maalum.<br>ii) Wanafunzi wasome habari hiyo kimya na kwa kasi na utulivu.<br>iii) Mwalimu awape wanafunzi maswali mbalimbali yakiwemo ya kufikirisha na ya kutolea maoni kutokana na habari waliyoisoma.<br>iv) Wanafunzi katika vikundi wajadili na wajibu maswali hayo kwa mdomo na kuandika. | Matini mbalimbali, vitabu | Je mwanafunzi ameweza kujibu maswali kutokana na habari aliyoisoma? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | d) Kufupisha habari aliyoisoma. | ...mawazo makuu... ...mtiririko wa mawazo ...kichwa cha habari... | ufupisho | i) Mwalimu kwa kutumia maswali na majibu, awaongoze wanafunzi wabaini mawazo makuu kutokana na habari waliyoisoma.<br>ii) Wanafunzi katika vikundi wajadili na kubaini mawazo makuu kutokana na habari waliyoisoma.<br>iii) Wanafunzi wafupishe habari waliyoisoma. | Makala mbalimbali, vitabu mbalimbali | Je mwanafunzi ameweza kufupisha habari aliyoisoma? | |
| 8.3. Kusoma kwa Burudani. | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kujenga tabia ya kujisomea | ...kuazima kitabu ...kurudisha kitabu | Maktaba, mchapishaji, mhariri | i) Mwalimu awaelekeze wanafunzi wasome maandiko mbalimbali.<br>ii) Wanafunzi wasome maandiko mbalimbali na kuyatolea taarifa kwa kuzingatia fani na maudhui, jina la kitabu, mwaka,mwandishi, mhariri, mchapishaji. | Vitabu vya kifasihi, magazeti, maandiko, makala mbalimbali. | Je mwanafunzi ameweza kujenga tabia ya kujisomea? | 4 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | NJIA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | iii)<br>iv) Mwalimu atunze kumbukumbu za usomaji wa wanafunzi wake. | | | |
| 8.4 Matumizi ya kamusi | Mwanafunzi aweze:<br>kubaini maana, matamshi na matumizi ya maneno kwa kutumia kamusi. | | | i) Mwalimu, kwa kutumia bungua bongo, awaelekeze wanafunzi wataje maneno kadhaa ya Kiswahili.<br>ii) Wanafunzi katika vikundi watumie kamusi kupata maneno hayo, maana zake, mtamshi na matumizi yake.<br>iii) Wanafunzi watumie maneno hayo katika sentensi au habari.<br>iv) Wanafunzi wasomeane sentensi/habari zao na wenzao wasahihishe matamshi. | Kamusi mbalimbali | Je, mwanafunzi ameweza kubaini maana, matamshi na matumizi ya maneno kwa kutumia kamusi. | 3 |

## KIDATO CHA TATU

### UMAHIRI

Somo la Kiswahili katika kidato cha tatu linatazamiwa kumpatia mwanafunzi ujuzi ufuataο:

1. Kuzungumza na kuandika kwa Kiswahili sanifu.
2. Kusoma na kuelewa habari ndefu za Kiswahili
3. Kusikiliza na kuelewa mazungumzo yaliyo katika lugha ya Kiswahili.
4. Kuandika habari ndefu kiasi kwa kuzingatia taratibu za uandishi.
5. Kubainisha na kutunga kazi za Fasihi andishi.
6. Kuhakiki kazi za fasihi andishi kwa kuzingatia vigezo vya uhakiki.
7. Kuainisha tungo.
8. Kueleza asili ya lugha ya Kiswahili.
9. Kueleza kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili katika enzi ya Waarabu nchini Tanzania.

### MALENGO

Mwanafunzi aweze:

(a) Kutunga kazi za kifasihi na za kiada kwa kutumia Kiswahili sanifu.
(b) Kuwasiliana kwa mazungumzo na maandishi na watu katika miktadha mbalimbali.
(c) Kusoma na kuelewa maandiko mbalimbali.
(d) Kusikiliza na kuelewa kwa kina taarifa au habari mbalimbali kutokana na vyanzo vya habari zinazohusu masuala ya jamii.
(e) Kusoma na kuhakiki kazi za fasihi andishi.
(f) Kuainisha na kuchanganua tungo.
(g) Kuielewa na kuieleza asili ya lugha ya Kiswahili.
(h) Kueleza kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili katika enzi ya Waarabu na Wajerumani nchini Tanzania.

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1.0 NGELI ZA NOMINO**<br><br>Kuzielewa Ngeli | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kufafanua upatanisho wa kisarufi katika sentensi. | | Ngeli, fasili kibarua kifaranga, ukuta, uta, njia, nyasi<br><br>Upatanisho | i) Mwalimu atumie maswali na majibu, mifano na majadiliano kuwaongoza wanafunzi kubainisha ruwaza ya upatanisho wa kisarufi baina ya maneno katika sentensi.<br>ii) Wanafunzi wajadili upatanisho wa kisarufi katika sentensi mbalimbali na kubainisha ruwaza yake.<br>iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi wachore jedwali lenye sentensi zenye upatanisho wa kisarufi. | Chati ya ngeli, matini zenye ngeli za majina.<br><br>Chati ya ngeli za nomini. | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua upatanisho wa kisarufi katika sentensi? | 14 |
| | | | | iv) Wanafunzi watunge sentensi na habari kwa kutumia upatanisho mwafaka.<br>v) Wanafunzi wafanye kazi mradi ya kukusanya sentensi ambazo zimekiuka upatanisho wa kisarufi katika maeneo yao na shuleni. Wazilete na kuzijadili darasani, kisha wazisahihishe. | | | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kuandika habari zenye upatanisho wa kisarufi. | | | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa njia ya onesho mbinu, watunge habari zenye upatanisho wa kisarufi<br>ii) Wanafunzi watunge sentensi mbalimbali kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi. | | Je mwanafunzi ameweza kuandika habari zenye upatanisho wa kisarufi? | |
| | b) Kubainisha virai na vishazi na sentensi katika tungo. | | | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi watumie orodha ya tungo kubainisha tofauti za tungo hizo.<br>ii) Wanafunzi wabainishe tofauti za tungo hizo kwa kuzingatia ukamilifu wa ujumbe unatolewa.<br>iii) Mwalimu atumie mifano kutambulisha virai, vishazi na sentensi. | | Je, mwanafunzi ameweza kubainisha virai na vishazi katika tungo? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **2.0 MJENGO WA TUNGO**<br>2.1 Kueleza Mjengo wa Tungo. | Mwanafunzi aweze<br>a) Kueleza dhima ya tungo. | | Tungo, virai, vishazi, ainisha | i) Kwa kutumia maswali na majibu, uchunguzi na majadiliano, mwalimu awaongoze wanafunzi wabaini tungo mbalimbali kutokana na mazungumzo na maandiko anwai.<br>ii) Wanafunzi wabaini tungo mbalimbali kutokana na mazungumzo na maandishi.<br>iii) Wanafunzi, wapange tungo hizo kwa kutofautisha zilizo na zisizo tungo halisi.<br>iv) Wanafunzi, wakiongozwa na mwalimu waeleze dhima ya tungo katika mawasiliano.<br>v) Wanafunzi katika vikundi wafanye mazoezi ya kubainisha tungo mbalimbali katika mazungumzo na maandishi. | Chati yenye tungo za virai, vishazi na sentensi maandiko mbalimbali. | Je, mwanafunzi ameweza kufasili tungo? | 4 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kubainisha virai na vishazi na sentensi katika tungo. | | | iv) Mwalimu awaongoze wanafunzi watumie orodha ya tungo kubainisha tofauti za tungo hizo.<br>v) Wanafunzi wabainishe tofauti za tungo hizo kwa kuzingatia ukamilifu wa ujumbe unatolewa.<br>vi) Mwalimu atumie mifano kutambulisha virai, vishazi na sentensi. | | Je, mwanafunzi ameweza kubainisha virai na vishazi katika tungo? | |
| 2.2 Ufafanuzi wa Aina za Tungo. | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kubainisha virai | Virai vya….<br>Virai…. | Virai vivumishi, virai vielezi, virai nomino. | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja tungo mbalimbali na ziandikwe ubaoni.<br>ii) Wanafunzi wakiongozwa na mwalimu wabaini aina mbalimbali za virai vilivyomo kwenye tungo hizo.<br>iii) Wanafunzi waorodheshe virai hivyo kulingana na aina zake. | | Je, mwanafunzi ameweza kubainisha virai? | 16 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kufafanua virai. | Kwa njia ya.... | | i) Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kufafanua aina za virai kulingana na dhima zake katika mawasiliano.<br>ii) Wanafunzi wajadili na kufafanua virai vya aina mbalimbali. | | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua virai? | |
| | c) Kufafanua aina za vishazi. | ... kwa njia ya .... | Kiima, kiarifu, kikundi nomino, kifungu tenzi, kikundi kielezi | i) Kwa kutumia chati ya tungo zenye vishazi, mwalimu awaongoze wanafunzi kubaini vishazi vilivyomo kwenye tungo hizo.<br>ii) Wanafunzi katika vikundi wajadili na kubaini aina za vishazi.<br>iii) Wanafunzi watumie vishazi hivyo katika sentensi n'a habari.<br>iv) Wanafunzi wafanye kazi mradi ya kuchunguza na kukusanya vishazi na kuvioanisha. | Chati ya tungo zenye vishazi. | Je, mwanafunzi ameweza kuainisha vishazi? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | d) Kuainisha sentensi | …sentensi sahili…… kishazi huru kishazi tegemezi… | Ainisha sahihi, changamano, shurutia ambatano | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kutunga sentensi mbalimbali na ziandikwe ubaoni.<br>ii) Mwalimu kwa kutumia chati yenye aina ya sentensi aulize maswali na wanafunzi wabaini aina za sentensi.<br>iii) Wanafunzi wakubainishe aina za sentensi. | | Je mwanafunzi ameweza kuainisha sentensi? | |
| | | | Kuchanganua, majedwali, vipashio matawi | i) Wanafunzi watunge sentensi kadhaa na mwalimu aziandike ubaoni.<br>ii) Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kuchanganua sentensi kwa njia ya matawi na majedwali.<br>iii) Wanafunzi wachanganue sentensi mbalimbali kwa njia ya majedwali. | Chati yenye aina za sentensi. mabango yenye majedwali ya uchanganuzi wa sentensi.<br>- kwa njia ya majedwali<br>- kwa njia ya matawi | Je, mwanafunzi ameweza kuchanganua sentensi kwa njia ya majedwali na matawi? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **3.0 MAENDELEO YA KISWAHILI**<br><br>3.1 Asili ya Kiswahili | a) Mwanafunzi aweze kuonesha ushahidi wa kimsamiati na kimuundo | | Ubantu<br>Visawe | i) Mwalimu kwa kutumia majadiliano na chati ya visawe, awaongoze wanafunzi kuonesha ushahidi wa kimsamiati na kimuundo wa Ubantu wa Kiswahili kwa kuzingatia llugha za makabila mbalimbali ya Tanzania.<br>ii) Wanafunzi watoe mifano kadhaa ya maneno kuthibitisha ubantu wa Kiswahili. Wafanye hivyo kwa kuzungumza na kwa kuandika.<br>iii) Wanafunzi wafanye utafiti wa maneno mbalimbali ya lugha za Kibantu na kuyahusisha na lugha ya Kiswahili kimuundo na kimsamiati. | i) Kamusi za Kiswahili<br>ii) Chati ya visawe vya maneno ya Kiswahili na maneno ya lugha nyingine za kibantu. | Je, mwanafunzi ameweza kuonesha mfanano wa kimsamiati wa Kiswahili na lugha nyingine za kibantu? | 8 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kufafanua jinsi miundo ya Kiswahili inavyofanana na miundo ya lugha nyingine za kibantu. | | Ruwaza | i) Mwalimu aongoze wanafunzi watamke sentensi moja kwa lugha mbalimbali za kibantu, kisha aongoze majadiliano kuhusu kufafana kwa sentensi hizo.<br>ii) Wanafunzi wajenge ruwaza kutokana na sentensi hizo.<br>iii)Mwalimu atumie chati ya ruwaza za miundo ya Kiswahili na lugha nyingine za kibantu kuongoza majadiliano ya mfanano huo.<br>iv) Wanafunzi wajadili kufanana kwa miundo hiyo.<br>v) Wanafunzi wafanye kazi mradi ya utafiti wa miundo mbalimbali ya Kiswahili na kuifananisha na ya lugha zao na nyingine za kibantu. | Chati ya ruwaza ya miundo ya Kiswahili na lugha nyingine ya kibantu. | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua mfano wa ruwaza ya miundo ya Kiswahili na ya lugha nyingine za kibantu? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 3.2 Kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania katika enzi ya Waarabu. | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kueleza ukuaji wa Kiswahili kimsamiati nchini Tanzania katika enzi ya Waarabu. | ….enzi ya …. | madarasa, kitabu, hakimu, sheria, | i) Kwa kutumia maswali na majibu na majadiliano mwalimu awangoze wanafunzi kubaini namna Kiswahili kilivyokuwa katika enzi ya Waarabu kimsamiati. Mwalimu awaongoze wanafunzi wachunguze chati ya maneno.<br>ii) Wanafunzi wajadili na kujibu maswali kivikundi.<br>iii) Wanafunzi katika vikundi wajadili njia mbalimbali zilizosaidia kukua kwa Kiswahili katika enzi ya Waarabu, kimsamiati.<br>iv) Wanafunzi wabaini mifano mbalimbali ya msamiati uliotokana na utawala wa Waarabu. | Chati ya maneno yenye asili ya Kiarabu.<br>Ramani ya Tanzania inayoonesha miji ya kwanza kukuza Kiswahili. | Je, mwanafunzi ameweza kueleza ukuaji wa Kiswahili kimsamiati katika enzi ya Waarabu nchini Tanzania? | 6 |
| | b) Kueleza kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania katika enzi ya Waarabu. | | | i) Kwa kutumia njia ya bunguabongo, majadiliano na maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza jinsi Kiswahili kilivyoenea katika sehemu mbalimbali nchini Tanzania.<br>. | Ramani ya Tanzania inayoonesha kuenea kwa Kiswahili enzi ya Waarabu. | Je, mwanafunzi ameweza kueleza kuenea kwa Kiswahili katika enzi ya Waarabu nchini Tanzania? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | ii) Wanafunzi wajadili na kueleza jinsi Kiswahili kilivyoenea sehemu mbalimbali na sababu zake wakati wa utawala wa Waarabu.<br>iii) Wanafunzi watumie ramani ya Tanzania kubainisha ueneaji wa Kiswahili enzi za Waarabu | | | 6 |
| 3.3 Kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania katika enzi ya Wajerumani | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kufafanua ukuaji wa Kiswahili nchini katika enzi za | Utawala wa … | | i) Mwalimu atumie maswali na majibu pamoja na majadiliano ya kubaini jitihada mbalimbali zilizofanywa katika kukuza Kiswahili hapa nchini wakati wa utalawa wa Wajerumani.<br>ii) Wanafunzi wajadili na kudurusu maandiko mbalimbali kuhusu juhudi zilizokuza Kiswahili wakati wa Wajerumani | | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua ukuaji wa Kiswahili nchini katika enzi ya Wajerumani. | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA | UPIMAJI | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kuhakiki maudhui katika riwaya, ushairi na tamthiliya | ….ujumbe wa<br>….falsafa ya.<br>…dhamira ya… | dhamira<br>maadili<br>Falsafa<br>ujumbe | i) Kwa kutumia vigezo vya maudhui mwalimu awaongoze wanafunzi kujadili maudhui katika riwaya, ushairi na tamthiliya.<br>ii) Wanafunzi katika vikundi wajadili na kubaini maudhui katika riwaya teule.<br>iii) Wanafunzi wahakiki maudhui katika riwaya, ushairi na tamthiliya zilizoteuliwa. | Matini mbalimbali za kifasihi, vitabu teule vya riwaya tamthiliya na ushairi. | Je, mwanafunzi ameweza kuhakiki mudhui ya riwaya ushairi, na tamthiliya? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kueleza kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania wakati wa utawala wa | | | i) Kwa njia ya bungua bongo, mwalimu aongoze wanafunzi waeleze jinsi Kiswahili kilivyoenea nchini katika enzi ya Wajerumani.<br>ii) Wanafunzi wadurusu maandiko pia wajadili jitihada za kueneza Kiswahiili nchini enzi za Wajerumani. | | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua ueneaji wa Kiswahili nchini wakati wa utawala wa Wajerumani? | 6 |
| **4.0 UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI ANDISHI**<br><br>4.1 Dhana ya uhakiki | | ...kazi za.....<br>.....kinga dhidi ya...<br>uhakiki wa .... | Uhakiki, fani, maudhui, miundo, ukimwi, ambukiza, kinga, toharisha. | Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi kueleza maana ya uhakiki. | | Je, mwanafunzi ameweza kueleza maana ya uhakiki? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 4.2 Uhakiki wa riwaya, tamthiliya na ushairi. | Mwanafunzi aweze: a) Kuhakiki fani katika riwaya, tamthiliya na ushairi. | Muundo wa… Vina vya…. Takriri kituo | Kimapokeo, wahusika mviringo/bapa, Vina, mizani, beti, kituo, tamathali za semi, upeo. | i) Mwalimu awaelekeze wanafunzi wasome vitabu teule vya riwaya tamthiliya na ushairi. ii) Mwalimu awaulize wanafunzi maswali ya jumla ya vitabu hivyo. iii) Wanafunzi wajibu maswali hayo kwa mdomo kisha kwa kuandika. iv) Kwa kutumia vigezo vya fani mwalimu awaongoze wanafunzi kujadili fani ya riwaya tamthiliya na ushairi katika vitabu vilivyoteuliwa. v) Wanafunzi katika vikundi wajadili na kubaini ubora na upungufu wa fani katika vitabu teule vya riwaya tamthiliya na ushairi. vi) Wanafunzi wahakiki fani katika riwaya, tamthiliya na ushairi teule. | Vitabu teule vya riwaya, tamthiliya na ushairi. Matini mbalimbali za kifasihi. | Je, mwanafunzi ameweza kuhakiki fani katika riwaya, tamthiliya na ushairi? | 20 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kuhakiki maudhui katika riwaya, ushairi na tamthiliya | ….ujumbe wa<br>….falsafa ya.<br>…dhamira ya… | dhamira maadili<br>Falsafa<br>ujumbe | i) Kwa kutumia vigezo vya maudhui mwalimu awaongoze wanafunzi kujadili maudhui katika riwaya, ushairi na tamthiliya.<br>ii) Wanafunzi katika vikundi wajadili na kubaini maudhui katika riwaya teule.<br>iii) Wanafunzi wahakiki maudhui katika riwaya, ushairi na tamthiliya zilizoteuliwa. | Matini mbalimbali za kifasihi, vitabu teule vya riwaya tamthiliya na ushairi. | Je, mwanafunzi ameweza kuhakiki mudhui ya riwaya ushairi, na tamthiliya? | |
| **5.0 UTUNGAJI WA KAZI ZA FASIHI ANDISHI**<br>5.1 Utungaji wa hadithi | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kupambanua mikondo ya hadithi. | …mtindo…<br>…upelelezi wa…<br>…historia ya…<br>…riwaya ya…. | mikondo<br>upelelezi<br>hadhira<br><br>mielekeo,<br>ujasusi, sira. | i) Mwalimu atumie maswali na majibu pamoja na majadiliano kubaini fasili ya hadithi.<br>ii) Wanafunzi wajadili na kujibu maswali ili kubaini fasili ya hadithi. | Mabango yenye picha za idadi ya watu, kudhibiti uhalifu ujasirimali. | Je, mwanafunzi ameweza kupambanua mikondo ya hadithi? | 8 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 5.2 Utungaji tamthiliya. | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kueleza dhima ya tamthiliya. | … lugha fasaha… | hadhira, dhamira, mandhari, jukwaa, jinsia igizo. | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kujadili fasili na dhima ya tamthiliya.<br>ii) Wanafunzi wajadili na kubaini fasili na dhima ya tamthiliya.<br>iii) Mwalimu awape wanafunzi matini fupi zenye tamthiliya kisha awaongoze wanafunzi waigize.<br>iv) Wanafunzi waigize tamthiliya hiyo. | Mabango yenye picha zenye maadili katika jamii. | Je, mwanafunzi ameweza kufasili tamthiliya? | 8 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | iii) Kwa kutumia mifano mwalimu awaeleze wanafunzi mikondo ya hadithi, ambayo ni ya mielekeo: kama vile: upelelezi, historia, ujasusi, sira.<br>iv) Wanafunzi katika vikundi wapambanue mikondo ya hadithi kutokana na riwaya mbalimbali walizosoma. | | | |
| | b) Kutunga riwaya fupi. | …riwaya<br>…<br>...msingi ya… | kazimradi, hadhira, dhamira, maadili, mandhari, muktadha. | i) Kwa kutumia chati ya misingi ya uandishi wa riwaya mwalimu awaelekeze mambo muhimu ya kuzingatia katika kuandika riwaya fupi.<br>ii) Wanafunzi katika vikundi wajadili na kubaini misingi hiyo. | Chati ya misingi ya uandishi wa riwaya. Mabango yenye picha za Elimu ya Mazingira, Ukimwi, umasikini. | Je, mwanafunzi ameweza kutunga riwaya fupi? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | iii) Wanafunzi wafanye, kazi mradi ya kuandika riwaya fupi:<br>Riwaya hizo zijumuishe taratibu za kuvuka barabara kwa usalama na utumiaji wa mantiki kulingana na mada husika.<br>iv) Riwaya fupi hizo ziwasilishwe na kujadiliwa darasani. | | | |
| 5.2 Utungaji tamthiliya. | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kueleza dhima ya | … lugha fasaha… | hadhira, dhamira, mandhari, jukwaa, jinsia igizo. | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kujadili fasili na dhima ya tamthiliya.<br>ii) Wanafunzi wajadili na kubaini fasili na dhima ya tamthiliya.<br>iii) Mwalimu awape wanafunzi matini fupi zenye tamthiliya kisha awaongoze wanafunzi waigize.<br>iv) Wanafunzi waigize tamthiliya hiyo. | Mabango yenye picha zenye maadili katika jamii. | Je, mwanafunzi ameweza kufasili tamthiliya? | 8 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **6.0 UANDISHI WA INSHA NA MATANGAZO**<br><br>6.1 Uandishi wa Insha za Kisanaa | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kueleza misingi ya kuandika insha. | ... za kisanaa... | utangulizi, kiini, hitimisho, mihemko, misongo, istilahi, aya, nyanja, tamathali za semi. | i) Kwa kutumia majadiliano, maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kubaini misingi ya uandishi wa insha za kisanaa.<br>ii) Wanafunzi wabaini misingi ya uandishi wa insha za kisanaa kwa kujibu maswali na majadiliano.<br>iii) Kwa njia ya bunguabongo na maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi wabaini misingi ya uandishi wa insha za kisanaa.<br>iv) Wanafunzi wajadili na kubaini misingi ya uandishi wa insha za kisanaa. | Picha zinazohusu madawa ya kulevya, Mazingira, usalama barabarani. | Je mwanafunzi ameweza kubaini misingi ya kuandika insha? | 5 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kutunga tamthiliya. | | | i) Kwa kutumia chati ya misingi ya uandishi wa tamthiliya mwalimu awaongoze wanafunzi kujadili mbinu za uandishi wa tamthiliya.<br>ii) Wanafunzi katika vikundi watumie chati ya misingi ya uandishi wa tamthiliya kujadili na kubaini misingi ya uandishi wa tamthiliya.<br>iii)Mwalimu awape wanafunzi kazi mradi ya kuandika tamthiliya. Tamthiliya hizo zijumuishe mada zifuatazo: uzungumzaji wa lugha fasaha, mgawanyo wa majukumu kijinsia, haki za mtoto, alama, michoro na ishara za usalama barabarani.<br>iv)Kazi hizo ziletwe darasani ili zijadiliwe na kutolewa maoni. | Chati ya misingi ya uandishi wa tamthiliya. Mabango yenye picha za Ukimwi, madawa ya kulevya, kanda za sauti zenye maigizo. | Je, mwanafunzi ameweza kutunga tamthiliya? | |

## KIDATO CHA NNE

### UMAHIRI

Baada ya kujifunza Kiswahili kidato cha Nne, wanafunzi watakuwa na ujuzi ufuatao:

1. Kuzungumza na kuandika kwa Kiswahili sanifu.
2. Kusoma na kuelewa habari ndefu kiasi za Kiswahili
3. Kusikiliza na kuelewa mazungumzo yaliyoko katika lugha ya Kiswahili.
4. Kuandika habari ndefu kiasi kwa kuzingatia taratibu za uandishi.
5. Kuchanganua sentensi.
6. Kubainisha na kutunga kazi za fasihi andishi.
7. Kuhakiki kazi za Fasihi andishi kwa kuzingatia vigezo vya uhakiki.
8. Kueleza kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili katika enzi ya Waingereza na baada ya uhuru nchini Tanzania.

### MALENGO

Baada ya kujifunza Kiswahili kwa kufuata muhtasari huu, mwanafunzi ataweza:

(a) Kuwasiliana kwa mazungumzo na maandishi na watu katika miktadha mbalimbali.

(b) Kusikiliza na kuelewa kwa kina taarifa au habari mbalimbali kutokana na vyanzo vya habari zinazohusu masuala ya ndani ya jamii.

(c) Kutunga kazi za kifasihi na za kiada kwa kutumia Kiswahili sanifu katika miktadha mbalimbali.

(d) Kuchanganua sentensi.

(e) Kusoma na kuhakiki kazi za kifasihi andishi.

(f) Kuelewa maumbo na tabia za maneno.

(g) Kuelewa na kueleza kukua na kuenea kwa Kiswahili katika enzi ya Waingereza na baada ya uhuru nchini Tanzania.

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1.0 KUONGEZA MSAMIATI WA KISWAHILI**<br><br>Uundaji wa Maneno | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kueleza mazingira yanayosababisha kuhitaji maneno mapya. | | Mwanajeshi, UKUTA,<br><br>UKIMWI, Deltao, shiganga, kitivo, kipera. Shati, Ngeli, Darasa, Mwanaharamu, mwanafunzi | i) Mwalimu atumie maswali na majibu na majadiliano kuibua miktadha inayodai maneno mapya.<br>ii) Wanafunzi wafanye majadiliano ya vikundi na kueleza mazingira yanayodai maneno mapya. | | Je, mwanafunzi ameweza kueleza mazingira yanayosababisha mahitaji ya mazingira yanayosababisha mahitaji ya maneno mapya? | 8 |
| | b) Kueleza njia mbalimbali za kuunda maneno. | | | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia maswali na majibu kueleza njia za kuunda maneno.<br>ii) Wanafunzi wataje njia hizo kwa mdomo na kwa kuandika. | Matini yenye maneno yaliyoundwa kwa njia tofauti tofauti. | Je, mwanafunzi ameweza kutaja njia mbalimbali za kuunda maneno? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | c) Kuunda maneno katika miktadha mbalimbali. | | | i) Mwalimu awangoze wanafunzi wabaini na wataje maneno ya Kiswahili yaliyoundwa kwa kutohoa na kubandika silabi.<br>ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi kuunda maneno kwa kutumia njia ya kutohoa na kubandika silabi.<br>iii) Wanafunzi katika vikundi waunde maneno kwa kubandika silabi na kutohoa kutoka lugha nyingine.<br>iv) Wanafunzi wayatumie maneno yaliyoundwa katika sentensi mbalimbali kwa mdomo na kwa kuandika. | | Je, mwanafunzi ameweza kuunda maneno kwa njia mbalimbali? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **2.0 UKUAJI NA UENEAJI WA KISWAHILI ENZI YA WAINGEREZA NA BAADA YA UHURU**<br>2.1 Ukuaji na Ueneaji wa Kiswahili Katika Enzi ya Waingereza. | a) Kueleza kuenea kwa Kiswahili katika enzi ya Waingereza nchini Tanzania. | ... kuenea kwa...<br>... enzi ya... | Sarufu, shanga, mtama, dini, kaptula, sime. | i) Kwa kutumia maswali na majibu na majadiliano na kuchunguza ramani ya Tanzania, mwalimu awaongoze wanafunzi kubaini kuenea kwa Kiswahili katika enzi ya Waingereza nchini Tanzania.<br>ii) Wanafunzi wajadili na kujibu maswali ya kubaini kuenea kwa Kiswahili katika enzi ya Waingereza nchini Tanzania. | Ramani ya Tanzania kuonesha vituo vya kupokea na kueneza Kiswahili: Zanzibar, Tanga Tabora, Mzizima (DSM), Ujiji. | Je, mwanafunzi ameweza kueleza kuenea kwa Kiswahili katika enzi ya Waingereza nchini Tanzania? | |
| 2.2 Ukuaji na Ueneaji wa Kiswahili Baada ya Uhuru | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kueleza shughuli mbalimbali zinazowezesha kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini. | | Dini, Elimu, biashara, utawala. | i) Mwalimu atumie majadiliano na bungua bongo kuongoza wanafunzi kueleza shughuli mbalimbali zinazowezesha ukuaji na ueneaji wa Kiswahili.<br>ii) Wanafunzi waeleze kwa mifano, shughuli za kijamii, kisiasa, kielimu zinazowezesha kuenea kwa Kiswahili. | | Je, mwanafunzi ameweza kufafanua shughuli zinazowezesha ukuaji na ueneaji wa Kiswahili nchini? | 10 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kueleza dhima za kila asasi inayokuza Kiswahili. | …kukuza Kiswahili<br>…Kueneza Kiswahili<br>…Kuchunguza Kiswahili…..<br>…Kuthamini Kiswahili…. | Asasi, ukuzaji usanifishaji taasisi | i) Kwa kutumia maswali na majibu na majadiliano na kuchunguza chati za asasi mwalimu awangoze wanafunzi kutaja asasi mbalimbali zinazokuza na kueneza Kiswahili nchini Tanzania, kama vile BAKITA, TUKI, UKUTA, TAKILUKI Taasisi ya Elimu Tanzania.<br>ii) Wanafunzi wajadili na kubaini asasi hizo.<br>iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika vikundi vya majadiliano na maswali na majibu kubaini dhima ya kila asasi ya kukuza na kueneza Kiswahili nchini Tanzania. | Chati ya asasi zinazokuza Kiswahili na dhima zake. | Je, mwanafunzi ameweza kueleza dhima za kila mojawapo ya asasi za Kiswahili? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | i) Wanafunzi wajadili na kubaini dhima za kila asasi za Kiswahili kwa mdomo na kwa kuandika. | | | |
| **3.0 UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI ANDISHI**<br><br>3.1 Uhakiki wa Ushairi, Tamthiliya na Riwaya.. | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kubaini taarifa muhimu za mwandishi wa kila kitabu. | | umahiri<br>umaarufu<br>malenga<br>msanii. | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi, kwa kutumia majadiliano, maswali na majibu, waeleze taarifa muhimu za maisha ya mwadishi wa kila kitabu.<br>ii) Wanafunzi watafute taarifa hizo kwa njia ya kazi mradi.<br>iii) Mwalimu aongoze majadiliano kuhusu taarifa za waandishi zilizokusanywa na wanafunzi. | Vitabu mbalimbali vya fasihi. | Je, mwanafunzi ameweza kueleza taarifa muhimu za waandishi wa vitabu vya fasihi? | |
| | b) Kuhakiki fani katika ushairi, riwaya na tamthiliya. | …diwani ya…<br>…tamthiliya ya..<br>…riwaya ya…. | fani, maudhui, muundo, mtindo, wahusika, mandhari, ujumbe, falsafa. | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa majadiliano wahakiki vipengele vya fani. | Vitabu teule vya riwaya, tamthiliya na ushairi.<br>Kanda za video za riwaya na tamthiliya. | Je, mwanafunzi ameweza kuhakiki fani katika ushairi, riwaya na tamthiliya? | 24 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | ii) Wanafunzi wachambue vipengele vya fani na kuvitolea kauli za kitathmini.<br>iii) Mwalimu atumie maswali na majibu kuvibaini vipengele vya kifani na jinsi ya kuvihakiki katika riwaya, ushairi na tamthiliya teule.<br>iv) Wanafunzi wahakiki fani katika riwaya, ushairi na tamthiliya teule | | | |
| | c) Kuhakiki maudhui katika ushairi, riwaya, na tamthiliya | …diwani ya…<br>…mashairi ya… | Diwani, tamathali za semi, tashibiha, sitiari, takriri, mizani, kituo, vina. | i) Kwa kutumia vipengele vya kuchambua maudhui mwalimu awaongoze wanafunzi kuchambua maudhui katika ushairi, riwaya na tamthiliya teule.<br>ii) Wanafunzi wahakiki maudhui katika riwaya, ushairi na tamthiliya teule. | Diwani/ vitabu teule vya ushairi, riwaya, na tamthiliya. | Je, mwanafunzi ameweza kuhakiki maudhui katika ushairi, riwaya na tamthiliya? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **4.0 KUTUNGA KAZI ZA FASIHI**<br><br>Utungaji wa Mashairi. | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kueleza kanuni za utungaji wa mashairi. | ...miundo....<br>....mapokeo...<br><br>...utungaji wa...<br>...urari wa... | mapokeo, urari, bahari, beti, silabi.<br><br>mizani, kituo, vina. | i) Kwa kutumia mifano ya mashairi mbalimbli ya kimapokeo mwalimu awaongoze wanafunzi kubaini taratibu za uandishi katika mashairi hayo.<br>ii) Wanafunzi katika vikundi wajadili na kubaini vipengele vinavyofanana au kutofautiana katika mashairi hayo.<br>iii) Mwalimu ahusishe vipengele hivyo na kanuni za utungaji wa mashairi.<br>iv) Wanafunzi wakiongozwa na mwalimu kubaini maana za istilahi zinazohusiana na kanuni za utungaji wa mashairi ya kimapokeo. | Matini mbalimbali za mashairi, tenzi na ngonjera.<br>Kanda za sauti zenye mashairi, tenzi na ngonjera zilizoimbwa na kuigizwa. | Je, mwanafunzi ameweza kueleza kanuni za utungaji wa mashairi ya kimapokeo? | 17 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | i) Wanafunzi katika vikundi wajadili istilahi hizo kwa kutumia mifano mbalimbali ya mashairi ya kimapokeo. | | | |
| **5.0 UANDISHI**<br>5.1 Kundika Insha za Kiada. | Mwanafunzi aweze kuandika insha za kiada (zisizo za kisanaa). | … insha za….<br>Uandishi wa….<br>...zisizo za kisanaa….za kisanaa. | kiada, utangulizi, kiini, hitimisho, aya, mpangilio. | i) Mwalimu awape matini kadhaa zenye insha mbalimbali.<br>ii) Wanafunzi katika vikundi wasome na kuzijadili na kubaini muundo wa insha hizo.<br>iii) Mwalimu awape wanafunzi mada kadhaa za kutunga insha. Mada hizo zijumuishe: Haki na fursa sawa baina ya jinsi, namna ya kuzungumza hadharani, njia za kuzuia maambukizi ya ukimwi. | | | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi wafanye majadiliano ya kubaini vidokezo muhimu vya uandishi wa insha.<br>ii) Wanafunzi watumie vigezo hivyo kuandika insha zenye maneno yasiyopungua 250. | Matini zenye insha zenye maudhui mbalimbali. | Je, mwanafunzi ameweza kuandika insha za kiada? | 6 |
| 5.2 Uandishi wa Hotuba | Mwanafunzi aweze kuandika hotuba. | ...kutoa hotuba...,<br>kiini cha....<br>Kwa niaba ya....<br>Mheshimiwa...<br>Ndugu ........<br>Shukurani zangu......<br>Natumia nafasi hii... | Hotuba, kiini cha hotuba, hitimisho | i) Kwa kutumia matini za hotuba na maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kubaini taratibu za uandishi wa hotuba.<br>ii) Wanafunzi wabaini taratibu hizo kwa kujibu maswali wakizingatia muundo wake. | Matini mbalimbali za hotuba. Kanda za sauti za hotuba mbalimbali na kinasa sauti. | Je, mwanafunzi ameweza kuandika hotuba? | 6 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kuandika hotuba.<br>iv) Wanafunzi waandike hotuba wakizingatia taratibu za uandishi wa hotuba; hotuba hizo zijumuishe mada hizi: Fasili ya ajira mbaya ya mtoto, dhana ya idadi ya watu athari za ajira mbaya ya mtoto<br>v) Wanafunzi wafanye mazoezi ya kutoa hotuba wakiongozwa na mwalimu. | | | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 5.3 Uandishi wa Risala | Mwanafunzi aweze kuandika risala | Risala ya….<br>Ndugu mgeni rasmi……<br>Mheshimiwa…<br>Imandikwa na….<br>Shukurani….. | Risala<br>Kiini cha risala,<br>hitimisho. | i) Mwalimu awape wanafunzi matini mbalimbali za risala.<br>ii) Wanafunzi katika vikundi wazichunguze, wajadiline na kubaini muundo wake.<br>iii) Kwa kutumia taratibu hizo za uandishi wa risala mwalimu awangoze wanafunzi kuandika risala.<br>iv) Wanafunzi waandike risala kwa kuzingatia taratibu za uandishi wa risala. | Matini za risala anuai.<br>Kanda za sauti zenye risala na kinasa sauti. | Je, mwanafunzi ameweza kuandika risala? | 6 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 5.4 Uandishi wa kumbukumbu za mikutano | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kuandika kumbukumbu za mkutano | …kumbukumbu za….<br>…ilikubaliwa…<br>…iliamuliwa…<br>…iliagizwa….<br>…imeidhinishwa na….<br>Imethibitishwa na… | kumbukumbu, ajenda, dondoo, yatokanayo, mengineyo | i) Mwalimu awape wanafunzi kivikundi matini mbalimbali za kumbukumbu za mikutano.<br>ii) Wanafunzi wajadili na kubaini muundo wa kumbukumbu hizo<br>.<br>iii) Mwalimu aandae mkutano wa mfano.<br>iv) Kila mwanafunzi aandike kumbukumbu za mkutano huo.<br>v) Mwalimu aongoze majadiliano kuhusu kumbukumbu zilizoandikwa kwa kuzingatia ubora na upungufu wa kumbukumbu hizo.<br>vi) Wanafunzi katika vikundi wajadili kumbukumbu zilizoandikwa wakizingatia ubora na upungufu wake.<br>vii) Wanafunzi wafanye mazoezi ya kuandika kumbukumbu za mikutano. | Matini mbalimbali za kumbukumbu za mikutano. | Je, mwanafunzi ameweza kuandika kumbukumbu za mikutano? | 6 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **6.0 UFAHAMU**<br>6.1 Ufahamu wa kusikiliza | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kujibu maswali ya habari aliyoisikiliza. | Ufahamu wa...<br>...kusikiliza kwa makini... | ufahamu | i) Mwalimu awasomee wanafunzi matini mbalimbali.<br>ii) Wanafunzi wasikilize kwa makini.<br>iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kujibu maswali kutokana na matini zilizosomwa.<br>iv) Wanafunzi wajibu maswali hayo kwa kuzungumza na kwa kuandika. | Matini zenye habari mbalimbali, taarifa, kanda na vinasa sauti. | Je, mwanafunzi ameweza kujibu maswali ya habari aliyoisikiliza? | 6 |
| | 2. Kufupisha habari aliyoisikiliza. | | Mawazo makuu ufupisho | i) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kutumia maswali na majibu kubaini mawazo makuu kutokana na habari walizosikiliza.<br>ii) Wanafunzi wabaini mawazo makuu kutokana na habari walizosikiliza kwa kuzungumza na kwa kuandika. | | Je, mwanafunzi ameweza kufupisha habari aliyoisikiliza? | |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | iii) Mwalimu awaelekeze wanafunzi wafupishe habari.<br>iv) Wanafunzi wafupishe habari walizosikiliza kwa urefu wa theluthi moja. | | | |
| 6.2 Ufahamu wa kusoma | Mwanafunzi aweze:<br>a) Kujibu maswali kutokana na habari ndefu aliyoisoma. | ..kusoma kwa makini.... | (Utokane na matini zitakazosomwa) | i) Mwalimu awape wanafunzi matini mbalimbali za ufahamu.<br>ii) Wanafunzi wazisome matini hizo kimya na kwa makini.<br>iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kujibu maswali kutokana na matini walizosoma.<br>iv)Wanafunzi wajibu maswali kutokana na matini walizosoma kwa mdomo na kwa kuandika. | Matini anuai za ufahamu | Je, mwanafunzi ameweza kujibu maswali kutokana na habari ndefu aliyoisoma? | 14 |

| MADA/MADA NDOGO | MALENGO MAHUSUSI | MIUNDO | MSAMIATI | MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA | ZANA/ VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b) Kufupisha habari ndefu aliyoisoma. | | | i) Kwa kutumia maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kubaini mawazo makuu katika matini walizosoma.<br>ii) Wanafunzi wabaini mawazo makuu kutokana na matini walizosoma kwa mdomo na kwa kuandika.<br>iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kufupisha habari.<br>iv) Wanafunzi wafupishe habari walizosoma kwa kuunganisha mawazo makuu waliyopata. | | Je, mwanafunzi ameweza kufupisha habari ndefu aliyoisoma? | |



91

Taasisi ya Elimu Tanzania